# UHUSIANO WA MIKAKATI YA UFUNDISHAJI WA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI NA UMILISI WA KUSOMA KATIKA SHULE ZA MSINGI, KASARANI, KAUNTI YA NAIROBI, KENYA


**NA**

**SELINA RHOBI CHACHA**

**E55/23475/11**


**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA ELIMU, SHULE YA ELIMU, CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**OCTOBER, 2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kingine kwa mahitaji ya shahada yoyote ile.

______________________________ ____________________

**Selina Rhobi Chacha** **Tarehe**

E55/23475/2011

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

______________________________ ________________

**Dkt. Hamisi O. Babusa.** **Tarehe**

Idara ya Elimu, Mawasiliano na Teknolojia

Chuo Kikuu cha Kenyatta

______________________________ ________________

**Prof. John Kimemia** **Tarehe**

Idara ya Elimu Mawasiliano na Teknolojia

Chuo Kikuu cha Kenyatta

## YALIYOMO

**UNGAMO** .......... **ii**
**YALIYOMO** .......... **iii**
**MAJEDWALI** .......... **vi**
**MICHORO** .......... **vii**
**VIFUPISHO VYA MANENO YALIYOTUMIWA** .......... **viii**
**SHUKURANI** .......... **ix**
**IKISIRI** .......... **x**
**ABSTRACT** .......... **xi**
**SURA YA KWANZA:UTANGULIZI** .......... **1**
1.1 Usuli wa utafiti .......... 1
1.2 Suala la utafiti .......... 4
1.3 Kusudi la utafiti .......... 5
1.4 Malengo ya utafiti .......... 5
1.5 Maswali ya utafiti .......... 5
1.6 Umuhimu wa utafiti .......... 6
1.7 Upeo na mipaka .......... 6
1.8 Tahadhania .......... 7
1.9 Misingi ya nadharia .......... 8
1.10 Kiunzi dhanifu .......... 12
1.11 Ufafanuzi wa istilahi .......... 14
**SURA YA PILI:YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA** .......... **15**
2.1 Utangulizi .......... 15
2.2 Maana ya fasihi ya watoto .......... 15
    2.2.1 Waliokusudiwa .......... 15
    2.2.2 Sababu ya kuandika .......... 16
    2.2.3 Mtindo na ubora wa fasihi .......... 16
2.3 Umuhimu wa kusoma fasihi ya watoto .......... 17
2.3 Umilisi wa kusoma .......... 20
2.4 Ufundishaji wa fasihi ya watoto .......... 21

2.4.1 Mikakati ya ufundishaji fasihi ........................................................22
2.5 Nafasi ya vifaa vya ufundishaji wa fasihi ........................................................ 24
2.6 Maandalizi ya walimu katika kufundisha fasihi ya watoto ............................. 24
2.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........................................................................... 25
2.8 Hitimisho ........................................................................................................... 28
**SURA YA TATU:MUUNDO NA NJIA ZA KUKUSANYA DATA ...............30**
3.1 Utangulizi ........................................................................................................... 30
3.2 Muundo wa utafiti ............................................................................................. 30
3.3 Vigeu vya utafiti ................................................................................................ 31
3.4 Eneo la utafiti..................................................................................................... 31
3.5 Wasailiwa lengwa .............................................................................................. 32
3.6 Sampuli na mchakato wa kuteua sampuli........................................................ 33
3.7 Njia na vifaa vya utafifi ...................................................................................... 35
3.7.1 Maswali ya hojaji kwa walimu.........................................................35
3.7.2 Mahojiano........................................................................................36
3.7.3 Kuchunguza namna somo linavyofunzwa darasani ...........................36
3.7.4 Kutathmini uhusiano wa fasihi ya watoto na kusoma........................36
3.8 Majaribio ya vifaa vya utafiti ............................................................................ 37
3.8.1 Uhalali ...........................................................................................37
3.8.2 Utumainifu .....................................................................................37
3.9 Ukusanyaji wa data............................................................................................ 38
3.10 Uchanganuzi wa data ....................................................................................... 39
3.11 Maadili katika utafiti ........................................................................................ 39
**SURA YA NNE:UCHANGANUZI WA DATA ..............................................40**
4.1 Utangulizi ........................................................................................................... 40
4.2 Demografia ya wahojiwa ................................................................................... 40
4.2.1 Usambazaji wa hojaji na mahojiano.................................................40
4.2.2 Jinsia ya walimu wa fasihi ...............................................................41
4.2.3 Umri wa walimu wa fasihi ...............................................................42
4.2.4 Kiwango cha elimu...........................................................................43

4.2.5 Tajiriba katika ufundishaji wa Kiswahili ..........................................44
4.2.6 Vipindi vya fasihi vilivyofunzwa kwa wiki .......................................45
4.3 Mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya kiswahili ............................... 46
4.4 Baadhi ya vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wa fasihi katika shule za msingi ............................................................................................................ 51
4.5 Umilisi wa kusoma fasihi miongoni mwa wanafunzi ..................................... 58
**SURA YA TANO:MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.......63**
5.1 Utangulizi ......................................................................................................... 63
5.2 Muhtasari .......................................................................................................... 63
5.2.1 Mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya kiswahili .................63
5.2.2 Baadhi ya vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wa fasihi katika shule za msingi ........................................................................64
5.2.3 Umilisi wa kusoma fasihi miongoni mwa wanafunzi .........................64
5.3 Hitimisho……………………………………………………..……………65
5.4 Mapendekezo ya utafiti...................................................................................... 66
5.4.1 Mapendekezo kwa walimu na Wizara ya Elimu ................................66
5.4.2 Mapendekezo kwa utafiti zaidi...........................................................67
**MAREJELEO........................................................................................................69**
**VIAMBATISHO...................................................................................................77**
Kiambatisho I: Hojaji ya walimu.............................................................................. 77
Kiambatisho II: Kutazama somo darasani ............................................................... 84
Kiambatisho III: Mwongozo wa maswali ya mahojiano na walimu wa kiswahili darasa la saba ........................................................................................................... 86
Kiambatisho IV: Matokeo ya uchambuzi wa insha za wanafunzi.......................... 88
Kiambatisho V: Barua ya idhini (NACOSTI) ....................................................... 89
Kiambatisho VI: Cheti cha idhini (NACOSTI) ..................................................... 90

# MAJEDWALI

Jedwali 1.1: Mfano wa matokeo ya Kiswahili katika mtihani wa KCPE, ya Kasarani ........ 3
Jedwali 3.1 Shule za kasarani zilizozingatiwa ........ 34
Jedwali 3.2 Wasailiwa katika utafiti ........ 35
Jedwali 4.1 Ripoti ya walimu kuhusu mikakati waliyotumia ........ 46
Jedwali 4.2 Kiwango cha Kujitayarisha cha Walimu Waliotumia Mitaala ya Somo la Fasihi ........ 50
Jedwali 4.3 Uzoefu wa vifaa vya ufundishaji wa fasihi vilivyotumiwa katika shule za msingi ........ 51
Jedwali 4.4 Ripoti ya walimu kuhusu uchaguzi wa vitabu shuleni ........ 56
Jedwali 4.5 Idadi ya vitabu kwenye maktaba ........ 57
Jedwali 4.6 Jinsi ya kutumia ubao kufundisha fasihi ........ 58
Jedwali 4.7 Alama za wanafunzi za insha zilizotathminiwa ........ 59
Jedwali 4.8 Utuzaji wa alama kwenye insha ........ 60
Jedwali 4.9 Kutuzwa kwa alama kwa kuzingatia sehemu ya uakifishaji na tahajia60
Jedwali 4.10 Alama kwa kuzingatia sehemu ya msamiati, uwasilishaji wa ujumbe na mpangilio na mtindo ........ 61

## MICHORO

Mchoro 1.1 Kiunzi dhanifu kinaonyesha vigeu huru, vigeu tegemezi na mambo yanayoathiri vigeu. .......... 12
Mchoro 4. 1 Uwakilishaji wa walimu wa fasihi kijinsia .......... 41
Mchoro 4.2 Uwakilishaji wa walimu wa fasihi kiumri .......... 42
Mchoro 4.3 Uwakilishaji wa walimu wa fasihi kulingana na kiwango cha elimu . 43
Mchoro 4.4 Tajiriba katika ufundishaji wa kiswahili .......... 44
Mchoro 4.5 Njia zinazowavutia wanafunzi nyakati za mafunzo ilivyripotiwa na walimu .......... 48
Mchoro 4.6 Ripoti ya walimu kuhusu changamoto za ufundishaji wa fasihi......... 49
Mchoro 4.7 Changamoto ya uteuzi wa vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wa fasihi ya watoto ilivyoripotiwa na walimu .......... 52
Mchoro 4.8 Jinsi wanafunzi walivyopewa zoezi la kusoma.......... 54
Mchoro 4.9 Wanaojumishwa kuwachagulia wanafunzi vitabu vinavyotumiwa shuleni.......... 55

## VIFUPISHO VYA MANENO YALIYOTUMIWA

| | | |
|---|---|---|
| KCPE | : | Mitihani wa Kitaifa wa Shule za Msingi |
| KICD | : | Taasisi ya Ukuzaji wa Mitala Nchini Kenya |
| KNEC | : | Baraza la Mtihani nchini Kenya |
| SPSS | : | Huduma ya Tarakilishi katika Uchunguzi wa Tarakimu |
| UNESCO | : | Shirika la Umoja wa Mataifa, na Elimu, Sayansi na Utamaduni. |

## SHUKURANI

Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Hamisi O. Babusa na Prof. John Kimemia kwa uongozi wao wa busara wakati nilipokuwa nikiufanya utafiti huu. Nawashukuru walimu katika Idara ya Mawasiliano na Teknolojia kwa usaidizi wao. Shukrani zangu za dhati pia ziwaendee walimu wakuu wa shule za Kasarani na walimu ambao walinifaa kwa maoni na katika ukusanyaji wa data za msingi. Kaadhalika , ningependa kumshukuru mume wangu Nyehita Maitaria na watoto wetu Ghati, Chacha, Bhoke na Mwita. Mungu awabariki.

# IKISIRI

Fasihi ya watoto ina manufaa katika ukuzaji wa umilisi wa lugha shuleni na hata katika mazingira ambayo si ya shule. Licha ya manufaa hayo, baadhi ya wanafunzi hawasomi vitabu vya hadithi. Kutopenda kusoma kunaweza kuwa kumesababishwa na mikakati inayotumiwa na walimu katika ufundishaji wa vitabu hivyo vya fasihi. Lengo la utafiti huu ni kuchanganua mikakati inayotumiwa katika ufundishaji wa fasihi na umilisi wa kusoma miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi za ya Kasarani. Utafiti huu ulichanganua vifaa vya kufundishia na kutathmini kazi ya wanafunzi. Aidha, utafiti uliongozwa na nadharia ya semiotiki ambayo hujengwa kwa miundo ishara. Mwanzilishi wa nadharia semiotiki alikuwa Charles Piece. Muundo wa utafiti huu ulikuwa wa usoroveya elezi. Mbinu bahatishi ilitumiwa kuteua shule za msingi za umma wilayani Kasarani. Mbinu kusudi ilitumiwa kuteua walimu wa Kiswahili kumi na wawili wanaofundisha darasa la saba. Mbinu bahatishi ilitumiwa kuteuwa wanafunzi sitini katika kila darasa. Insha sitini za wanafunzi katika shule ziliteuliwa na kuchanganuliwa ili kutathmini umilisi wa kusoma miongoni mwa wanafunzi. Vifaa vilivyotumiwa katika utafiti ni hojaji na mahojiano kwa walimu, kutazama somo darasani na kutathmini insha za wanafunzi. Data ilichanganuliwa kwa kutumia tarakilishi, ili kupata uwiano na wastani. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa kutumia maelezo, majedwali na michoro. Kutokana na utafitii, asili mia moja ya walimu waliripoti kuwa kusoma kwa kimya na wa kipekee ni mikakati mikuu wanayoitumia kufunza fasihi. Utafiti pia ulibaini kuwa, asili mia moja ya walimu walitumia vitabu vya hadithi na ubao katika ufundishaji. Vifaa vya teknolojia ya kisasa havikutumiwa. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa wanafunzi hawakufanya vizuri katika insha zao kwasababu walimu hawakutumia mikakati tofauti tofauti na vifaa vya teknolojia ya kisasa. Walimu wanatakikana kutumia mikakati tofauti tofauti na vifaa vya teknolojia ya kisasa katika ufundishaji ili kuimarisha matokeo ya lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwa walimu, wanafunzi, wakuzaji mitaala na watafiti wa fasihi ya watoto.

## ABSTRACT

Children literature is an important aspect in children's language performance in school and life after school. Despite its critical role, pupils are not reading enough literature books for them to master language. The purpose of this study was to analyse the teaching strategies used to teach children literature and reading competence among class seven pupils at Kasarani Sub-County, Nairobi County. The study aimed at achieving the following objectives: to analyse the teaching strategies used by teachers to teach children literature; to analyse resources used in teaching children literature; and to evaluate children's reading comptence in literature. This research was guided by Semeotic Theory. The design of the study was descriptive survey. Simple random sampling was used to sample twelve schools in Kasarani and purposive sampling was used to select twelve Kiswahili teacher's handling children literature in class seven. Questionnaires, interview guides, observation and document analysis were used to collect data. The collected data was edited, organized, entered into a computer and analyzed with the aid of Social Package for Social Sciences (SPSS). The analysed data was presented using descriptive statististics such as tables, graphs and charts. The findings of this study indicated that silent and individual reading were the major strategies used in teaching liteature in most primary schools, thus, teachers did not use variety of teaching strategies. All teachers (100%) agreed that story books and writing boardswere the major resources used in delivering children literature. The study concludes that new instructional techniques such as redio lessons, televisions, recorded videos and audios were not utilized at all. Majority of pupils, as well, did not perform well in all sections of composition.This is because the teachers did not use different strategies and new instructional techniques in their teaching to improve pupils performance. The study recommends that; teachers should use different strategies in teaching children's literature, children should be encouraged to read more story books, and library lessons should be more than one.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa utafiti

Lugha ya Kiswahili ina mchango mkubwa katika kubainisha malengo muhimu ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni, kijamii na kielimu miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki. Jambo hili limeipa hadhi lugha ya Kiswahili kiasi cha kutambulika miongoni mwa lugha saba za kimataifa katika karne ya ishirini na moja (Mbaabu, 1996 na King'ei, 2012). Lugha hizi ni Kiingereza, Kijerumani, Kirusi, Kireno, Kichina, Kihispaniola na Kiswahili.

Kulingana na Katiba ya Kenya (2010), Kiswahili ni lugha rasmi na ya taifa. Hii ni kutokana na serikali kutambua dhima yake katika maendeleo ya nchi. Kwa hivyo, Kiswahili ni chombo muhimu katika mawasiliano miongoni mwa jamii. Kwa mfano, asilimia themanini ya watu nchini Kenya huitumia lugha hiikatika mawasiliano yao ya kila siku. Uwiano huu umetambuliwa na shirika la Kimataifa la UNESCO (Momanyi, 2007).

Lugha ya Kiswahili ina vipengele vya msingi vinavyopaswa kuzingatiwa katika mawasiliano ya kijamii. Kwa hivyo, fasihi yake haiwezi kamwe kutenganishwa na lugha hii ya Kiswahili. Mfumo wa Elimu wa 8-4-4 nchini Kenya ulipoanzishwa mwaka wa 1985, Fasihi ya Kiswahili ilianza kupata nafasi ya kufundishwa katika shule za msingi, ambapo Kiswahili kilikuwa somo la lazima na la kutahiniwa katika shule zote za msingi na sekondari nchini Kenya. Aidha, mwaka wa 2002 wakuuza mitaala nchini walipendekeza kuhusisha somo la fasihi na somo la lugha

kuanzia darasa la kwanza hadi la nane. Hii ilitokana na ile hali ya kutaka kukuza stadi za lugha, tamaduni za kusoma na pia kujenga mielekeo chanya kuhusu fasihi na lugha ya Kiswahili.

Usomaji wa fasihi huweza kuimarisha stadi ya usomaji miongoni mwa wanafunzi. Kwa sababu, stadi ya kusoma huweza kumtayarisha mwanafunzi ili kuelewa na kufasiri yale anayoyasoma. Mwanafunzi anapofundishwa kusoma fasihi, anatarajiwa kuelewa anachokisoma, kupanua msamiati wake ambao pia hujikita katika stadi muhimu zinazozingatiwa. Kwa mfano, sarufi ambayo ni uti wa mgongo wa lugha yoyote huimarika pale ambapo mwanafunzi anaposoma vitabu vya hadithi.

Stadi ya kuandika ina uhusiano wa karibu sana na kusoma. Mwanafunzi anavyosoma maandishi au matini katika vitabu hivyo, ndivyo huweza kuimarisha uandishi wake. Kusikiliza na kuongea ni stadi ambazo pia zinauhusiano na kusoma kwa sababu usomaji unahusu usikivu na uelewaji, iwapo mwanafunzi atasoma kwa sauti (KICD, 2002).

Baadhi ya tafiti ambazo zimewahi kufanywa kuhusu kitengo cha usomaji wa fasihi zimeonyesha, walimu wamekuwa wakiwafundisha wanafunzi mbinu za kuwatayarisha ili kuweza kupita mtihani wa kitaifa wa Kiswahili. Mbae (2004) anasema kuwa, walimu wanazingatia zaidi vitabu vya kiada. Kwa hivyo, usomaji wa fasihi katika shule za msingi nchini Kenya umekuwa haupewi uzito unaostahili. Hali hiyo huweza kujenga mazingira hasi katika usomaji wa fasihi ya

watoto (Ngugi, 2009). Kwa sababu ni vigumu kwa wanafunzi kuweza kutumia vitabu hivyo kwa namna inavyostahili. Kuna uwezekano kwamba, mikakati inayotumiwa katika ufundishaji wa fasihi na kutokuwahusisha zaidi wanafunzi ndiko huweza kuwafanya wanafunzi kujijengea mwelekeo hasi kuhusu usomaji wa fasihi ya watoto.

Matokeo ya mtihani wa KCPE ya Kiswahili yamekuwa ya kiwango cha chini ya wastani katika miaka ya 2009 hadi 2012 katika ya Kasarani, Kaunti ya Nairobi. Hayo yamewasilishwa katika Jedwali 1.1.

**Jedwali 1.1: Mfano wa matokeo ya Kiswahili katika mtihani wa KCPE, ya Kasarani**

| Mwaka | Idadi ya wanafunzi waliofanya Mtihani | Alama ya Wastani |
|---|---|---|
| 2009 | 3692 | 46.02 |
| 2010 | 3539 | 47.73 |
| 2011 | 3290 | 46.98 |
| 2012 | 3688 | 46.21 |

***Asilia**: Mkuu wa Elimu wa ya Kasarani (2015)*

Ahmad na Aziz (2009), wanasema kuwa wanafunzi wengi hawaimudu lugha. Wanaendelea kusema kuwa hii inaweza kuwa ni kwa sababu ya mikakati inayotumiwa katika ufundishaji. Fasihi ni chombo muhimu cha kuboresha usomaji kwa kuwa huathiri sarufi, insha na ufahamu. Vipengele hivyo hutahiniwa katika mtihani wa KCPE. Matokeo kama hayo yanahitaji kutafutiwa suluhisho la kuboresha hakika katika ufundishaji wa usomaji wa vitabu vya hadithi.

Licha ya manufaa ya usomaji wa vitabu vya hadithi baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi hawapendi kusoma vitabu vya hadithi. Huenda kutopenda kusoma vitabu hivi kumechangiwa na mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto. Hayo yameungwa mkono na Mbae, (2004) anaposema kwamba, shule na mbinu za walimu  za kutegemea vitabu vya kiada zimechangia katika kutopenda kusoma kwa wanafunzi wa shule za msingi na za upili. Wanafunzi hawasomi vitabu vya kutosha (Ngugi, 2009). Wanafunzi ambao hawasomi vitabu vya hadithi vya kutosha hawawezi kuimudu lugha. Wanafunzi hao hawafanyi vizuri katika kiwango cha mtihani wa KCPE. Maoni hayo yamesisitiziwa na KNEC (2011) inapopendekeza kuwa, walimu wahimize wanafunzi wasome vitabu vya ziada ndiposa waweze kupita mtihani wao wa KCPE. Utafiti huu ulilenga kuchanganua mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili na umilisi wa kusoma , katika shule za msingi wilayani Kasarani.

### 1.2 Suala la utafiti

Usomaji wa vitabu vya hadithi una manufaa katika ukuzaji wa umilisi wa lugha ya Kiswahili katika viwango mbalimbali  vya masomo nchini Kenya. Usomaji huu huwa na uhusiano na stadi zote za kujifunza lugha ya Kiswahili. Mwanafunzi asipoimudu lugha hawezi kufanya vizuri katika mtihani wa somo la Kiswahili. Wanafunzi katika shule za msingi Kaunti ndogo ya Kasarani hawapiti vizuri mtihani wao wa Kiswahili wa KCPE. Matokeo yao yamekuwa chini ya wastani kutoka mwaka wa 2009 hadi 2012. Kuna uwezekano kwamba wanafunzi wanaposoma vitabu vya fasihi huchangia katika kuinua kiwango chao cha lugha. Utafiti huu ulichanganua mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili

katika shule za msingi Kaunti ndogo ya Kasarani ili kutafuta njia za kuinua matokea ya mtihani wa Kiswahili Katika shule za msingi Kaunti ndogo ya Kasarani.

**1.3 Kusudi la utafiti**

Kusudi la utafiti huu lilikuwa kutathmni uhusiano kati ya mikakati ya ufundishaji wa fasihi na umilisi wa kusoma  lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa darasa la saba katika shule za msingi Kasarani, Kaunti ya Nairobi.

**1.4 Malengo ya utafiti**

Madhumuni ya utafiti yalikuwa:

(i) Kutathmini uhusiano uliopo kati ya fasihi ya watoto na umilisi wa kusoma.

(ii) Kuchanganua mikakati inayotumiwa na walimu katika ufundishaji wa fasihi ya watoto.

(iii) Kufafanua vifaa vya ufundishaji vinavyotumiwa na walimu katika fasihi ya watoto.

**1.5 Maswali ya utafiti**

(i) Kuna uhusiano kati ya mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto na umilisi wa kusoma na kusoma?

(ii) Ni mikakati gani inayotumiwa na walimu katika ufundishaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili katika shule za msingi?

(iii)Walimu hutumia vifaa gani vya ufundishaji katika kufundisha fasihi ya Kiswahili ya watoto?

## 1.6 Umuhimu wa utafiti

Wanafunzi watafaidika kutokana na mikakati na vifaa vya ufundishaji ambavyo vitakuwa vimependekezwa kutokana na utafiti huu.

Matokeo ya utafiti huu yatasaidia kuihimiza Wizara ya Elimu kuandaa mafunzo kwa walimu kuhusu mbinu mwafaka za kufundisha lugha na fasihi ili kuimarisha umilisi wa kusoma lugha. Walimu wa Kiswahili watakuwa na motisha ya kutumia mikakati tofauti tofauti katika ufundishaji wa kusoma fasihi ya watoto ya Kiswahili katika shule za msingi.

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, Wakuza Mitaala nchini Kenya (KICD) wanaweza kuanda warsha na makongamano ambayo yatawahusisha walimu wa Kiswahili katika shule za msingi. Katika vikao hivi, walimu wataweza kuchangia na kujadiliana kuhusu mikakati inayofaa kushirikishwa katika ufunzaji wa fasihi.

## 1.7 Upeo na mipaka

Utafiti huu ulikuwa ukishughulikia uhusiano wa mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto na umilisi wa usomaji miongoni mwa wanafunzi wa darasa la saba tu katika shule teule. Mtafiti hakuzingatia shule ambazo ni za kibinafsi. Kwa sababu, shule hizo huwa na vifaa tofauti na zile za serikali. Kwa mfano, baadhi ya shule za kibinafsi huwa na vitabu vingi kuliko zile za serikali na baadhi huwa hazina vitabu kabisa. Shule za umma hupewa pesa na serikali kupitia wizara ya elimu za kununua vifaa vinavyokaribiana.

Shule hizo za umma zilizozingatiwa ziliteuliwa kwa kutumia mbinu bahatishi kuchagua shule kumi na mbilikatika Kaunti ndogo ya Kasarani na wanafunzi wa darasa la saba walishirikishwa. Madarasa kuanzia la kwanza hadi la sita hayakuzingatiwa katika utafiti huu. Kimsingi, wanafunzi hao wamekuwa wakisoma vitabu vya fasihi lakini kilele cha ujuzi huo hushuhudiwa katika darasa la saba. Darasa la nane huzingatia zaidi mazoezi ya marudio ili kuweza kujiandaa vilivyo katika mtihani wa kitaifa. Kwa maoni ya mtafiti ni kwamba, haikuwa vizuri wakisumbuliwa.

Utanzu wa fasihi ya watoto ndio ulizingatiwa. Kwa sababu, wanafunzi wa darasa la saba bado walitakikana kuwa wanasoma fasihi ya watoto. Utafiti huu uliwazingatia walimu wa Kiswahili wa darasa la saba katika shule teule za msingi katika Kasarani, Kauti ya Nairobi. Kwa sababu, katika darasa la saba wanafunzi waliofunzwa vizuri kusoma waliweza kujengewa mazingira yanayofaa ili kuweza kuwa na umilisi wa usomaji.

Utafiti huu pia ulichunguza mikakati inayotumiwa katika ufundishaji wa kusoma na ujifunzaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili ili waweze kuwa na umilisi wa usomaji.

## 1.8 Tahadhania

(i) Walimu hutumia mikakati inayofaa katika ufundishaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili.

(ii) Wanafunzi huweza kusoma na kuelewa wanachokisoma.

(iii) Wanafunzi hujisomea wenyewe somo la fasihi darasani.

(iv) Walimu hawapewi mafunzo mwafaka kuhusu fasihi ya watoto katika vyuo vya walimu.

## 1.9 Misingi ya nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya semiotiki. Nadharia hii huihakiki lugha ambayo hujengewa kwa miundo ya ishara. Ishara hizo ni huwa ni kiungo muhimu baina ya mwalimu na wanafunzi. Katika mawasiliano, ishara hizo za lugha huungana pamoja ili kuunda miundo teule katika lugha inayopatikana katika miundo teule inayorejelewa. Mwanzilishi wa nadharia hii ni Charles Pierce (1839-1914) aliyesema kuwa, semiotiki ni taaluma inayoshughulikia vipashio vilivyopo kama ishara katika lugha. Hata hivyo, nadharia ya semiotiki ilidokezwa hapo awali na mwanaisimu Ferdinard de Saussure (1857-1913) ambaye aliweka wazi ishara hizo katika miundo ya lugha. Kwa kufafanua miundo ya lugha, aliweza kutofautisha dhana ya kiashiria na kiashiriwa kwamba: kiashiria, matini au mifumo ya maneno haiwezi kueleweka yenyewe kwa kuzingatia matumizi yake katika muktadha wa mahusiano yake na viashiria vingine kama anavyoeleza Scholes (1974). Kwa hivyo, miundo ya lugha hujenga ruwaza ya kielezo cha kudhihirisha taratibu za kijamii.

Kabla ya Charles Pierce, wanamiundo walishikilia kuwa fasiri ya maana za kauli auujumbe hupatikana katika mfumo au ruwaza ya lugha. Mtazamo huo ulikuwa wenye upungufu wa dhima ya ishara zinazopatikana katika mfumo au muundo wa lugha. Katika matini za kifasihi, nadharia hiyo inaweza kuwa ni jambo ambalo

linajenga mazingira ya kutafakariili kuweza kuhusishwa na kiashiriwa katika jamii.

Katika ufundishaji wa fasihi, mwalimu anahitaji kuwaelekeza wanafunzi kutambua vipengele muhimu vilivyotumika katika utunzi na uwasilishaji. Kadhalika, wasomaji wa fasihi wataweza kuhusisha yale yanayowasilishwa na Tajiriba yao.

Maandishi katika vitabu vya fasihi hutumia maneno au kauli kama ishara za uwasilishaji. Maandishi hayo huwa yenye maana dhahirina batini. Umuhimu wake hutokana na matumizi ya lugha inayobuniwa na mwandishi kwa watoto. Nadharia hii inaakisi miundo mahususi ya lugha inayopatikana katika mawasiliano ya jamii. Naye Nagler (1974), ameichangia nadharia hii kwamba, mifumo hiyo ya maneno inapotumiwa ipasavyo, huweza kurutubisha ujumi siyo tu kwenye vitabu vya fasihi bali pia katika tanzu mbalimbali za fasihi.

Vipengele vya nadharia ya kisemiotiki katika utafiti huu vitatumiwa kufafanulia nafasi ya vipengele mahususi vya lugha katika utunzi na uwasilishaji wa vitabu vya hadithi za watoto. Kwa kuzingatia hayo, stadi mbalimbali zinazotumiwa katika ufundishaji wa fasihi ya watoto zitaweza kubainishwa. Kwa sababu vipengele hivyo vya nadharia hii ni vingi, mtafiti alijumuisha baadhi yavyo ili kujenga nguzo mahususi iliyotumiwa katika uchanganuzi wa data zilizozingatiwa. Aidha, nadharia ya semiotiki ilichangia katika utafiti huu kwa ambavyo vitabu vya fasihi hutumia ishara kama vile picha ambazo huwafurahisha

wanafunzi wa kiwango cha shule za msingi kuelewa mikakati inayotumiwa katika uwasilishaji na ufasiri wa matini zilizotumika.

Katika vitabu vya hadithi, yaliyomo au madhumuni huwa na uhusiano na tamaduni za watunzi walioziandika na wapokezi walioandikiwa. Hawkes (1977), anafafanua kwamba kila ishara, yaani matumizi ya matini kitendo ambacho huchochea tafakari ya mtu kurejelea au kupatanisha na muktadha wa kijamii. Aliyosisitiza Hawkes ni kwamba, viashiria vinavyotumiwa na wanajamii hujengeka katika misingi inayoweza kufafanuliwa na kufasiriwa. Matumizi ya viashiria hayawezi kutenganishwa na miktadha ya utamaduni na uhalisia wa jamii. Kwa hivyo, vitabu vya fasihi vinavyotumia katika shule za msingi huweza kumsaidia mwanafunzi katika umilisi wa kusoma na kutokana na yale yaliyomo na yale yanayopatikana katika uhalisi wa maisha yao.

Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki, mihimili yake ilikuwa ifuatavyo:

(i) Ishara zina miundo maalumu ya kisarufi. Ishara za lugha zinaweza kuwa ni kauli au neno moja ambapo kwa kushirikiana na ishara zingine huweza kuunda mfumo wa ruwaza ya maneno.

(ii) Ishara, yaani matini zitumikazo katika fasihi, huweza kuwa ni za moja kwa moja au za kiistiari. Iwapo ni ishara za kiistiari, ufafanuzi wake hujikita katika miktadha ya kitamaduni na uhalisia wa jamii. Ishara ya moja kwa moja hueleweka kwa urahisi katika Tajiriba ya watu au jamii.

(iii) Ishara hutumiwa katika miktadha ya ishara zingine. Matumizi ya ishara moja hayana maana iwapo hayakutumiwa sambamba na ishara zingine.

(iv) Ishara teule zinazotumiwa katika vitabu vya hadithi ni vipengele vya lugha ambavyo hujirejelea na ni rahisi kutambulika na kukumbukwa katika kazi yoyote ya fasihi.

(v) Ishara hutumiwa kuwasilisha ujumbe katika kazi maalumu ya fasihi kwa kuzingatia utamaduni wa watu.

Nguzo ya nadharia ya semiotiki iliunufaisha utafiti huu kwa utumiaji wa vitabu vya fasihi ya watoto katika kujengea mazoea ya kusoma Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi. Picha au taswira ambazo huibuliwa katika vitabu hivyo vya fasihi ni ishara zinazoweza kufasiriwa vyema kwa kuzingatia vipengele vya utamaduni na uhalisia katika jamii. Kwa uelekezi huo mbinu zinazotumika katika ufundishaji na ushirikishaji wa wanafunzi wa somo la fasihi zitatambuamuhimu katika usomaji na ujifunzaji wa vitabu vya fasihi miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi.


Mihimili iliyozingatiwa katika utafiti uliofanywa ilikuwa ni ifuatayo:

- Muundo wa kauli huwasilishwa kwa kuzingatia viashiria elekezi kama vile viakifishi.
- Kutokana na matumizi teule ya tamathali za usemi kama ishara huhitaji usaili na utafakari wa kufikia ujumbe batini (fiche) unaowasilishwa katika fasihi.
- Ujumbe unaowasilishwa huweza kufafanuliwa kwa kuzingatia muktadha ulioibuliwa na msanii na kupatanishwa na utamaduni na uhalisi wa maisha ya wanafunzi.

- Matini zinazotumika katika uwasilishaji wa fasihi hujengwa kwa ishara zinazotambuliwa na zinazoweza kufasiriwa.

## 1.10 Kiunzi dhanifu

Mihimili ya dhana inaonyesha uhusiano wa kati ya mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi ya Kiswahili na umilisi wa kusoma katika shule za msingi Nairobi. Kiunzi dhanifu cha dhana katika Mchoro1.1 kinaonyesha uhusiano wa vigeu huru na vigeu tegemezi. Vigeu huru huviathiri vigeu tegemezi ili kuleta matokeo ya utafiti ambayo ni umilisi wa kusoma. Kuna mambo ambayo yanaweza kuviathiri vigeu hivyo ili kuleta matokeo tofauti.




**Mchoro 1.1 Kiunzi dhanifu kinaonyesha vigeu huru, vigeu tegemezi na mambo yanayoathiri vigeu.**

**Asilia:** Mtafiti

Jedwali hili linabainisha kigeu tegemezi kimoja ambacho ni umilisi wa kusoma miongoni mwa wanafunzi.  Vigeu huru ni vitatu muhimu: mikakati ya ufundishaji, kutathmini kazi ya wanafunzi, vifaa vya ufundishaji,na kutathmini kazi ya wanafunzi. Vigeu vyote hivi vinauhusiano na mwalimu ambaye anaweza kumfanya mwanafunzi ajenge mwelekeo chanya au hasi katika usomaji wa vitabu vya fasihi.

Mwalimu akitumia mikakati isiyofaa katika ufundishaji huenda wanafunzi hawatakuwa wametayarishwa au kuandaliwa vilivyo katika usomaji ambao utaleta matokeo mema ya mtihani na aweze kujimudu katika stadi za lugha. Endapo vifaa havikutumiwa ipasavyo wanafunzi wanaweza kukosa kupenda kusoma na washindwe kutamka maneno yaliyoandikwa.

Darasani, mwalimu huchukuliwa kuwa ndiye chanzo cha kumfanya mwanafunzi awe na mwelekeo hasi kuhusu kusoma vitabu vya fasihi ya watoto. Kuna mambo ambayo yanaweza kuathiri usomaji kama vile mielekeo ya wanafunzi,  idadi ya vipindi, motisha na uraibu wa mwanafunzi. Mikakati inayofaa inapotumika katika ufundishaji, huenda wanafunzi wakapenda kusoma na kuwa na umilisi wa kusoma. Iwapo  mwalimu atazingatia hayo, ufundishaji wa usomaji wa fasihi ya watoto utakuwa wenye manufaa. Kwa sababu, matokeo hayo yatakuwa ni kusoma na kuelewa, wanafunzi wataweza kutumia viakifishi kwa usahihi, wataweza kuwa waandishi bora na kuwasilisha hoja zao kwa njia mwafaka katika insha na pia kukuza na kutumia msamiati kwa njia ya usahihi.

## 1.11 Ufafanuzi wa istilahi

**Fasihi:** Hii ni sanaa itumiayo maneno ili kueleza kuhusu maisha na Tajiriba za binadamu.

**Fasihi ya watoto:** Aina ya fasihi iliyoandikwa kwa kuwazingatia watoto kama hadhira lengwa.

**Kusoma:** Kudurusu maandishi yanayopatikana katika vitabu.

**Mikakati:** Njia mahususi zinazotumiwa katika darasa ili kuelekeza wanafunzi.

**Ufundishaji:** Kitendo cha kutoa mafunzo ili kuweza. Kuwaelekeza wanafunzi.

**Ujifunzaji:** Kitendo cha kupokea mafunzo kwa wanafunzi ili waelewe.

**Umilisi:** Kupata ufahamu au ujuzi wa lugha na ufasiri wake.

**Usomaji:** Kitendo cha kuwasilisha yaliyoandikwa kwa kuzingatia matamshi.

**Vitabu vya kiada:** Vitabu vinavyotumiwa na wanafunzi kulingana na wizara ya elimu.

# SURA YA PILI

# YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia mambo yanayohusu ufundishaji wa fasihi ya watoto katika shule za msingi. Mambo hayo ni kama vile: maana ya fasihi ya watoto, umuhimu wa kusoma fasihi ya watoto, ufundishaji wa fasihi, tamaduni ya usomaji , uteuzi wa vitabu vya fasihi, yaliyoandikwa kuhusu mada, vifaa vya ufundishaji na viwango vya elimu vya walimu.

## 2.2 Maana ya fasihi ya watoto

Katika kutoa maana ya fasihi ya watoto mambo matatu muhimu yalizingatiwa, walioandikiwa, sababu ya kuandika, na mtindo na ubora wa fasihi. Mambo haya ndiyo yatakayotoa ufafanuzi wa fasihi ya watoto kulingana na utafiti huu.

### 2.2.1 Waliokusudiwa

Fasihi ya watoto imetolewa fasiri mbalimbali. Kwa mfano Weinreich na Bartlett (2000), wameeleza kuwa katika fasihi ya watoto, hadhira hiyo ya watoto lazima iwe ndiyo inayomfanya mwandishi kukiandika na kukiwasilisha kitabu hicho cha fasihi. Naye Hunt (1996), amefasiri dhana ya fasihi ya watoto kuwaile inayolenga kiwango cha mtoto kama msomaji wa fasihi hiyo. Kwa hivyo, msomaji wa vitabu vya fasihi huwa ni watoto au mtoto aliyeandikiwa. Vile vile, hii ni kazi ya sanaa ambayo husomwa na watoto katika jamii yoyote.

Oberstein (1996) ameifafanuafasihi ya watoto kuwa, ni vitabu ambavyo vina uhusiano wa karibu na wale wanaovisoma. Anaendelea kwa kusema kuwa, fasihi hii pia huwekwa pamoja na vifaa vingine ambavyo si lazima viwe kama umbo la kitabu.

### 2.2.2 Sababu ya kuandika

Ghosn (2003) ameeleza kuwa, vitabu vilivyoandikiwa watoto vinatakikana kuwafurahisha badala ya kusomwa kwa minajili ya mtihani. Vitabu vya kusomwa ili wanafunzi watahiniwe huandikwa kwa mtindo unaofuata kanuni na utaratibu mahususi. Kwa kurejelea hilo, Hollindale (1997) amesema kuwani kazi yote ya fasihi ya watoto humfanya mtoto kuyaangazia na kuinasibisha na maisha yake ili aweze kuyatafakari na kujenga mtazamo ufaao kuhusu maisha.

Vile vile Mpesha (1995)ameielezafasihi ya watoto kwa kuzingatia sababu ya kuandika fasihi hiyo kuwa; lengo muhimu la vitabu pamoja na maandishi yote yanayosomwa na mtoto ni kuweza kumfurahisha.

### 2.2.3 Mtindo na ubora wa fasihi

Lukens (1995), ameangazia fasihi ya watoto kwa kuzingatia mambo mengi ambayo hudhihirika katika fasihi hiyo. Kwa mfano: uhalisi katika hadithi, mambo yanayokumbukwa, ukweli katika maudhui yanayobainishwa, wahusika na mtindo mwepesi wa kisanaa unaotumiwa katika kutayarisha fasihi hii ya watoto. Mambo hayo huwa ni sheria na vigezo vinavyopasa kuzingatiwa katika kuandika fasihi ya watoto.

## 2.3 Umuhimu wa kusoma fasihi ya watoto

Baadhi ya wataalamu wa kifasihi wanakariri kuwa vitabu vya fasihi vinapowiana na maisha ya mwanafunzi anayevisoma. Kwa mfano Mwanzi, (1982) na Brooks na Huck, (1979) wameeleza kuwa vitabu hivyo hukuza na kuimarisha akili ya mtoto kisaikolojia, kijamii na pia kuibulia fikira ya uelewa wa dunia wanamoishi. Wanafunzi hao wanaposoma vitabu hivyo, huwafanya kuelewa zaidi tamaduni za watu katika jamii zao na zile za jamii zinginezo. Kwa hivyo, hujenga uelewa zaidi kwa kuzingatia kuwa watu wengine wana mawazo na hisia kama zao. Wanaposoma wanapata dira ya kuwaelekeza katika kukabiliana na maisha ya sasa. Collie na Slater (2000) wamekariri kuwa, fasihi ya watoto hukuza lugha kwa wanafunzi hasa wanaosoma vitabu vya fasihi kwa wingi. Kwa hivyo, fasihi hii huwawezesha kuwa na umilisi wa msamiati. Kwa mfano, mwanafunzi aliye na msamiati mwingi huweza kujimudu katika mazungumzo na kujieleza kikamilifu.

Hurst na Johns (2004) na Davis (1990) wameonyesha uhusiano uliopo kati ya fasihi ya watoto na masomo mengine yanayoshugulikiwa na watoto. Kwa mfano, Hurst ametaja vitabu ambavyo vinatumiwa kufundisha Historia, Jiografia, Hisabati na Elimu Jamii miongoni mwa zingine. Vitabu hivyo vina manufaa katika masomo mengine yanayoshughulikiwa na watoto. Vinatumiwa katika kuelimisha hadhira ya wanafunzi kuhusu mambo katika masomo mengine. Wanafunzi wanapovisoma, huweza kuwasaidia katika usomaji wa matini nyinginezo zinazotumiwa katika uwasilishaji wake. Tajiriba yao ya usomaji huweza pia kuongezeka. Kwa mfano, Ngugi (2009) anaeleza kuwa fasihi hiyo ya watoto husaidia katika uelewaji wa

masomo mengine na pia katika kukuza tamaduni ya kusoma. Musau na Chacha (2001), wamefafanua baadhi ya sababu zinazotumika katika ufundishaji wa fasihi kama chombo kinachompatia mwanafunzi jicho la upekuzi. Kwa hivyo, hadhira inapopekuwa yale yaliyomo katika vitabu hivyo huelemikia, huburudika na pia huliwazika.

Kwa mujibu wa Mpesha (1995) fasihi ya watoto katika jamii yoyote ile ambayo hulenga kuwafahamisha watoto kuhusu mambo mabaya, hisia na matarajio ya jamii hiyo. Aidha, anasema kuwa, kitabu kinachowafaa watoto ni kile kinachomwezesha msanii kuwasiliana moja kwa moja na hadhira ya watoto anaowashughulikia. Kitabu hicho kiwe kinachohusu Tajiriba ya watoto katika jamii zao. Mambo hayo ni kama vile majukumu, miiko na maadili. Ameeleza kuwa, fasihi hiyo ni chombo kilicho na nguvu kwa jamii, na wala si maandiko yanayohusu ukweli wa jamii tu bali pia ni chombo cha mawasiliano katika jamii. Kwa hiyo, wanafunzi wanapovisoma hukuza mwelekeo mwafaka kwa kutambua umuhimu wa kusoma makala na vitabu vingi vya fasihi ya Kiswahili. Hii huwafunza maadili na kubeza uovu katika muktadha wa jamii za kiafrika. Watoto hufunzwa maadili ili jamii iweze kuendeleza kizazi kilicho na maelewano mema. Maudhui hayo huwasilishwa kwa uelekezaji wa watoto. Weche (2000), amechangia kuwa fasihi ya watoto ni kioo cha kumwongoza mtoto katika mambo yanayohusu maadili. Pia anasema kuwa, fasihi hiyo inapaswa kukashifu tabia zisizokubalika na kubainika katika jamii. Kadri wanafunzi wanaposoma vitabu hivyo, ndivyo huweza kupata mafunzo muhimu kuhusu maadili ya jamii. Mawazo

hayo yamekaririwa pia na Karuga (2005) anaeleza kuwa, fasihi hiyo ni mwigo wa fasihi ya watu wazima. Kwa hivyo, huchukuliwa kama chombo cha kuwafundishia watoto maadili na kuwafurahisha.

Silabasi ya Kiswahili (2002), inahimiza kuwa fasihi katika mfumo wa elimu ambayo husaidia mwanafunzi katika lugha na ambayo hupanua mawazo na kumfanya kufurahia uandishi wa kila aina. Kwa sababu, mtoto hutumia lugha katika muktadha wa mawasiliano na wengine. Kwa kufanya hivyo, somo la Kiswahili linatakikana kujenga msukumo wa kusoma fasihi ya Kiswahili. Fasihi hii husaidia katika maingiliano ya wao kwa wao miongoni mwa wanafunzi.

Taasisi Ya Ukuzaji Wa Mitaala Nchini (KICD) hutoa uelekezi kupitia kwa mwongozo wa kitabu cha 'The Orange Book' ambacho kina orodhaya vitabu vilivyoidhinishwa kutumiwa katika kila daraja la masomo. Taasisi hiyo imefanya hivyo kutokana na umuhimu wa somo hili la fasihi kwa wanafunzi wa shule za msingi. Kwa hivyo, somo la maktaba lipo wanafunzi waweze kufundishwa somo hilo la fasihi. Mwaka wa 2002, Taasisi ya Ukuzaji wa Mtaala Nchini (KICD) ilitoa toleo la silabasi mpya ambayo ilihusisha mafunzo ya fasihi na lugha ya Kiswahili kuanzia darasa la kwanza hadi la nane. Kuhusishwa huku kunatarajiwa kumwezesha mwanafunzi kukuza stadi ya kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Kwa hivyo, silabasi ya Kiswahili ilitilia mkazo umuundo ili kuwapa wanafunzi uwezo wa kumilisi lugha wanayoisoma. Fasihi ya watoto huweza kuwapa nafasi mwafaka ya kutumia lugha katika muktadha wa mawasiliano unaotarajiwa.

### 2.3 Umilisi wa kusoma

Masuala kuhusu usomaji yamefanyiwa utafiti na wasomi kwa muda mrefu kuhusu usomaji wa watu wazima (Chakava, 1994; Mbae, 2004; Bindra, 2007 na Ngunjiri, 2007).Waandishi hawa wanasema kuwa watu wengi nchini Kenya hawapendi kusoma. Aidha, wanasema watu wengi katika jamii huwa hawasomi zaidi ya kusoma magazeti. Usomaji huu wa magazeti hauwezi kuchangia katika kujenga tamaduni hiyo ya usomaji. Kwa mfano, Chakava (1994), ameangazia kuhusu baadhi ya wasomaji waafrika ambao hawasomi baada ya kumaliza shule.Inapobidi, husoma kwa malengo ya ajira. Anaendelea kuzungumzia kuhusu wanafunzi ambao wamemaliza shule za upili wakiulizwa wataje baadhi ya vitabu walivyovisoma katika maisha yao. Katika muktadha huu, wanaohusika hutaja tu vitabu vya fasihi walivyojifunza darasani.

Mfumo wa elimu nchini Kenya umekuwa ni tatizo kwa utamaduni wa kusoma kwa sababu mfumo huu huhimiza tu usomaji wa kupita mtihani. Watu wengi huwa wanajikita katika usomaji wa vitabu vya kiada. Kahenya, (1992) amechukulia kuwa vitabu vya kiada huogopesha watu kusoma badala ya kuwafurahisha. Kwa hivyo watu huwa ni wavivu wa kusoma afadhali watazame mchezo wa kuigiza au kutazama vipindi katika runinga badala ya kusoma vitabu.

Flavia (2011), ameangazia mazoea ya kusoma nchini Kenya. Katika tathmini yakeu tamaduni wa kusoma miongoni mwa wanafunzi na wazazi wao haujaimarika. Hii imetokana na mambo kama vile umasikini, njia potovu za

ufundishaji wa fasihi na ukosefu wa vitabu hivyo maktabani. Kwa hivyo, si watu wengi ambao huvipata vitabu hivyo ili kuvisoma.

Batambuzi (2007) amesema kuwa, watu hawawezi kujengewatamaduni ya kusoma pale ambapo hakuna cha kusomwa. Anaendelea kusema kuwa, halitakuwa jambo la maana kuwa na maktaba pale ambapo hakuna vitabu vya kusomwa. Wasomi wanahitaji kuamua vitabu wanavyovitaka pale maktabani. Konrad (2008) anaposema kuwa, mfumo wa elimu umetawaliwa na mitihani ambayo huwa na kigezo maalumu cha kuamua maisha ya baadaye ya mwanafunzi.

### 2.4 Ufundishaji wa fasihi ya watoto

Odaga (1985), ameshughulikia suala la ufundishaji wa fasihi na amefafanua kwamba, mchango wa walimu ni muhimu katika ufundishaji wa fasihi ya vijana. Amesema kuwa, walimu na shule wajishughulishe kwanza katika kujenga mwelekeo ufaao ndipo kutakuwa na mabadiliko katika hali ya usomaji.

Kitabu cha 'The Orange Book' kina orodha ya vitabu ambavyo vimeteuliwa ili viweze kutumiwa katika katika kila daraja la masomo. Taasisi hiyo imefanya hivyo ili kuwaongoza walimu na wanafunzi kuchagua vitabu vya fasihi vinavyowafaa.Walimu wanapochagua kitabu chochote kile cha kusomwa lazima kiwe ni miongoni mwa orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa na kupatikana katika kitabu cha 'The Orange Book'. Kwa hivyo, mfumo wa elimu ya 8-4-4 nchini Kenya ni tatizo kwa usomaji wa fasihi. Kwa sababu,umekuwa ukihimiza usomaji

wa kupita mtihani. Konrad (2008) amesema kuwa, mfumo wa elimu huweza kuamua maisha ya baadaye ya mwanafunzi.

Osazee (2004) amekariri kuwa, mfumo wa elimu katika bara la Afrika umejikita katika vitabu vya kiada ambavyo huzuia usomaji wa kujiburudisha. Mfumo huo ndio ulio nchini Kenya ambao huwafanya wanafunzi wasipende kusoma. Mwaka wa 2002, Wizara ya Elimu kupitia Taasisi ya Wakuza Mitaala Nchini Kenya (KICD) ilitoa silabasi ambayo ilihusisha fasihi ya Kiswahili kufundishwa na lugha ya Kiswahili kuanzia darasa la kwanza hadi nane. Mkazo huo ulikuwa kwenye kufundisha vipengele vyote vya fasihi kama vile ngano, mashairi na nyimbo.

Ngugi (2009), ameangazia swala hili la ufundishaji wa fasihi kwa kusema kuwa vitabu vya fasihi visiwepo tu kwa watoto bali vifundishwe ili kuwafanya wanafunzi wapende kuvisoma kwa furaha. Shule ambazo hukuza tamaduni za usomaji miongoni mwa wanafunzi huwafanya sio tu kufurahi bali pia kukuza viwango vyao vya lugha.

### 2.4.1 Mikakati ya ufundishaji fasihi

Ni muhimu kutilia mkazo mikakati ya ufundishaji wa fasihi ndipo usomaji wake uwe na manufaa kwa walengwa. Wasomi wengi wameangazia kuhusu mikakati tofauti tofauti inayotumiwa katika ufundishaji wa fasihi. Kwa mfano Ruddell (2002), amependekeza mikakati ifuatayo mahususi inayopaswa kuzingatiwa.

#### 2.4.1.1 Kusoma kwa sauti

Hii ni njia ya zamani ya kuwasomea wanafunzi kwa sauti. Mwalimu anaweza kuwasomea wanafunzi au mwanafunzi mmoja anaweza kusoma wengine wakisikiliza. Kusoma kwa sauti huwasaidia katika kujenga hali ya utulivu na usikivu. Aidha, huwasaidia wanafunzi katika kupenda lugha na kuhadithia hadithi inayosomwa.

#### 2.4.1.2 Kusimulia hadithi

Hii ni njia iliyotumiwa tangu zamani ya kusimulia hadithi bila kutumia maandishi. Chamber (1980), amekariri kuwa mikakati hii miwili, kusoma kwa sauti na kusimulia hadithi ndiyo husaidia wanafunzi kuwa na hamu na kuibua ile hamu ya kusoma. Hadithi inaweza kusimuliwa na mwalimu kwa wanafunzi au mwanafunzi anaweza kusimulia wanafunzi wenzake wakisikiliza.

#### 2.4.1.3 Usomaji wa kimya

Njia hii huhusisha usomi wa kimya kimya. Kila siku au wakati wa somo la fasihi. Kila mmoja wa wanafunzi na mwalimu wao husoma kimya kimya kwa dakika tano hadi kumi na tano. Katika usomaji huo, wanafunzi huchagua wanachotaka kusoma.

#### 2.4.1.4 Fasihi ya majadiliano katika makundi

Katika mkakati huu wanafunzi wa fasihi hujadiliana kwa kutumia usomaji wa pamoja katika kujifunza fasihi.Wanafunzi wanaojadiliana huwa watano au sita

darasani. Kila kikundi hujadiliana kuhusu matini tofauti. Kila mmoja katika kikundi hugeuka wanapobadilishana majukumu.Majukumu haya ni kama msimamizi wa majadiliano, anayeandika muhtasari na atakaye toa ripoti ya waliyojadiliana.

## 2.5 Nafasi ya vifaa vya ufundishaji wa fasihi

Vifaa vya ufundishaji ni sehemu muhimu katika utaratibu wa ufunzaji na ujifunzaji vinapotumiwa vizuri. Ayot (1986) anasema kuwa, vifaa vya ufundishaji ni zana za kufundisha na kujifunza zinazowasaidia walimu katika ufundishaji na huimarisha ujifunzaji. Mawazo haya yanaungwa mkono na Wright (1976) anaposema kuwa vyombo vya kufunza na kujifunza ni muhimu sana kwa sababu wanafunzi hupata habari zaidi kutokana na vyombo hivi kuliko kutoka kwa mwalimu. Mwalimu anapopanga atakayofunza, mikakati ya ufundishaji lazima aambatishe vifaa vya kufundisha ambavyo huhusisha somo atakalofundisha.

Kwa mujibu wa Sauders (1974), Tajiriba ndio msingi mkuu katika hatua za ujifunzaji. Anataja kuwa mtu hukumbuka asilimia 10 ya anayoyasikia, asilimia 50 ya anayoona na kuyasikia, asilimia 90 ya anayoona,anayosikia na anayoyatenda.

Ufundishaji unaofaa ni ule unaohuhusisha zaidi matumizi ya vifaa vya ufundishaj ambavyo huimarisha mwanafunzi.

## 2.6 Maandalizi ya walimu katika kufundisha fasihi ya watoto

Maandalizi ya walimu katuka vyuo vya walimu ni muhimu. Kwa sababu walimu ndio msingi katika ufundishaji darasani. Sifuna (1991) anasema kuwa, muundo thabiti wa mafunzo ya walimu ni muhimu katika kukuza mageuzi katika mfumo.

Anaendeleo kusema kuwa kutokufaulu kwa mageuzi ya elimu hutokea kwa sababu ya mafunzo duni wanayopata walimu vyuoni. Kwa mfano, baadhi ya walimu hawapati mafunzo ya kufundisha fasihi ya watoto (Ngugi, 2009). Hata kama mitaala na vifaa vimepangwa vizuri na walimu hawajapatiwa mafunzo yakutosha madhumuni ya mitaala hiyo hayatatimizwa.

**2.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Utafiti wa Ruthiiri (2012) umeshughulikia ufaafu wa vitabu vya kusoma kwa madarasa ya tano na sita katika shule za msingi. Maelezo yaliyotolewa ni kuwa, vitabu ambavyo huteuliwa kusomwa na wanafunzi wa madarasa hayo havifuati vigezo muhimu vilivyoidhinishwa. Aidha, lugha iliyotumiwa katika baadhi ya vitabu huwa na makosa ya kisarufi kama vile baadhi ya sentensi huwa ndefu sana hili huonyesha kutokuzingatia sifa zinazofaa katika uteuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto. Mawazo hayo yatanufaisha utafiti huu kwa sababu yalishughulikia vigezo vinavyotumiwa kuteuwa vitabu katika shule za msingi nchini Kenya, hasa darasa la saba linaloshughulikiwa. Kwa sababu, darasa hili huwa ni kilele cha mkusanyiko wa yaliyopitiwa katika usomaji wa wanafunzi

Ngugi (2009), ametafiti kuhusu hali ya fasihi ya watoto nchini Kenya. Ameshughulikia fasihi ya watoto hao katika usomaji. Kwa kuzingatia sababu zinazowafanya wanafunzi wasipende kusoma fasihi. Kazi yake imetofautiana na hii imetafitiwa, kwa sababu utafiti huu unatathmini uhusiano uliopo kati ya ufundishaji wa fasihi na umilisi wa usomaji hasa kwa kuhusisha mikakati ya

ufundishaji wa fasihi katika darasa la saba,vifaa vinavyotumiwa, mafunzo ya mwalimu na uteuzi wa vitabu vya hadithi.

Utafiti wa Muthubi (2005) umezingatia mikakati na mbinu za usimilishwaji katika fasihi ya watoto ameeleza kuwa mwandishi hana budi kuzingatia mbinu zinazofaa za usimilishwaji iwapo anatarajia kuibuka na kazi ya kiwango cha juu na iliyofanikiwa katika kuwafaa walengwa. Kazi yake imechangia utafiti huu kwa ambavyo ameshughulikia mbinu za usimilishwaji. Utafiti huu ulishughulikia mikakati inayotumiwa katika ufundishaji wa vitabu hivyo ambavyo vingi ni vilivyosimilishwa.

Gituku (1990), ameshughulikia vipera vya fasihi simulizi. Amechunguza namna vipengele vya ufundishaji wa kimawasiliano kutoka katika maigizo ya watoto ya kienyeji kama njia inayofanya ufundishaji wao katika shule za msingi. Utafiti wake ulitoa mwelekeo kwa utafiti uliofanywa kwa sababu maigizo ya watoto ya kienyeji ni njia ya kufundisha fasihi ya watoto. Mbali na hayo, utafiti unaoshughulikiwa utaangalia mikakati mingine ambayo hutumiwa wakati mwalimu anapofundisha fasihi ya watoto ya Kiswahili ili wanafunzi wawe na umilisi wa usomaji.

Eldreadge na Butterfield (1986), walifanya utafiti wa utumiaji wa vitabu vya fasihi ya watoto katika kufundisha usomaji. Matokeo ya utafiti wao ulibainisha kuwa utumiaji wa vitabu hivyo katika kufundisha kusoma huwa wenye manufaa kwa kujenga mwelekeo ufaao kwa wanafunzi. Utafiti ulioshughulikiwa ulifafanua

baadhi ya vipengele muhimu vya usomaji wa vitabu vya fasihi katika kudhihirisha nguvu na udhaifu wa mbinu zitumikazo shuleni.

Odaga (1985), ametafiti kuhusu fasihi ya watoto nchini Kenya. Amesema kwamba, fasihi ya watoto imepitia hatua mbalimbali katika kukua na kuendelea kwake. Alichotilia mkazo ni kuzingatia mambo muhimu katika nyanja zote za fasihi kama vile matumizi ya lugha inayolingana na kiwango cha mtoto. Utafiti huo ulikuwa na uhusiano na utafiti huu uliofanywa kwa kuzingatia mikakati ya ufundishaji ambayo inazingatia fasihi ya watoto.

Benton na Fox (1985), walishughulikia ufundishaji wa fasihi ya watoto kwa ujumla kwa kuwashughulikia watoto wa miaka tisa hadi kumi na minne. Walichunguza upokezi wa watoto katika tanzu za hadithi na ushairi. Matokeo ya uchunguzi wao ni kuwa watoto hupenda kujinasibisha na wahusika katika hadithi walizozisoma kwa kiwango kikubwa. Isitoshe, wamezungumzia watoto kutoka mazingira tofauti na wale wanaoshughulikiwa katika utafiti huu.

Hata hivyo, umri wa watoto walioshughulikiwa ni sawa kwani wanafunzi wa darasa la saba wengi huwa na umri kati ya miaka kumi na mitatu na kumi na minne. Utafiti huo uliufaa utafiti huu kwa sababu mbinu za ufundishaji wa fasihi zilishughulikiwa. Utafiti uliofanywa ulishughulikia uchanganuzi wa mikakati ya ufundishaji wa fasihi na umilisi wa kusoma.

Ray (1970), amehakiki kazi za kinjozi zinazowavutia watoto kati ya miaka tisa hadi kumi na mitatu. Ametoa mapendekezo kuhusu vitabu vinavyotakikana

kuwekwa maktabani ili vitumiwe na watoto walio katika kiwango hicho cha umri. Ameeleza vile vitabu vinavyofaa na kuwavutia wanafunzi hao huweza kuchaguliwa. Utafiti huo uliufaa utafiti huu kwa sababu vitabu vinavyosomwa na watoto lazima viteuliwe kwa makini ili viweze kutimiza malengo ya ufundishaji na umilisi wa kusoma

**2.8 Hitimisho**

Watafiti mbalimbali wameshughulikia mazoea ya usomaji wa fasihi ya watoto katika kupitia vitabu na tasnifu zilizoandikwa sikupatana na aliyeangazia. Uchanganuzi wa mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili na umilisi wa kusoma katika shule za msingi.

Usomaji wa vitabu vya fasihi ya watoto umeangaziwa na baadhi ya tafiti na imebainisha kuwa wanafunzi wa shule za msingi za Nairobi hawasomi vitabu vya fasihi vya kutosha ili kuwawezesha kuimudu lugha ya Kiswahili. Tafiti hizi hazikuangazia uhusiano uliopo baina ya mikakati ya ufundishaji, vifaa vinavyotumiwa na walimu wanapofundisha.

Baadhi ya tafiti za awali zimezingatia umuhimu wa fasihi ya watoto. Suala hili liliangaziwa kwa ujumla ambapo fasihi ina uhusiano wa moja kwa moja na mazingira ya mtoto.

Tafiti hizi hazikuzingatia mambo hasa yanayoathiri ufundishaji na umilisi wa kusoma katika shule za msingi. Utafiti huu ulichanganua mikakati na vifaa vinavyotumiwa na walimu katika ufundishaji wa fasihi ya watoto katika shule za

msingi. Kiini hasa cha utafiti huu ni kufafanua baadhi ya sababu muhimu zinazoathiri umilisi wa kusoma miongoni mwa wanaffunzi katika shule za msingi, Kasarani, kaunti ya Nairobi.

# SURA YA TATU

# MUUNDO NA NJIA ZA KUKUSANYA DATA

## 3.1 Utangulizi

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchanganua mikakati inayotumiwa na walimu wa shule za msingi wanapofundisha fasihi ya watoto ya Kiswahili na umilisi wa usomaji katika lugha ya Kiswahili. Aidha, utafiti huu ulizingatia muundo wa utafiti, vigeu vya utafiti, wasailiwa lengwa, mchakato wa kuteua sampuli, njia na vifaa vya utafiti, majaribio ya vifaa vya utafiti, ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

## 3.2 Muundo wa utafiti

Muundo wa usorovea elezi ulitumiwa. Kulingana na Kombo na Tromp (2006) ni kwamba, muundo huohutumiwa kupata data kuhusu mielekeo, maoni, mazoea na pia mambo muhimu yanayohusu elimu na maswala ya jamii. Katika utafiti huu muundo wa usorovea elezi kwa kuchunguza ulisaidia katika kupata habari zaidi kuhusu mikakati ya ufundishaji, mielekeo ya wanafunzi na walimu kuhusu ufundishaji na usomaji wa fasihi ya Kiswahili. Good (1972), ameeleza kuwa kwa kutumia muundo huu wa usorovea elezi, mtafiti anaweza kupata data ya kutathmini njia mbalimbali zinazotumiwa ili uamuzi mwafaka kuweza kufikiwa. Kwa kutumia muundo huo mtafiti aliweza kupata habari kamili kuhusu mikakati ambayo walimu wanaitumia kwa kufundisha usomaji wa fasihi katika shule za msingi.

## 3.3 Vigeu vya utafiti

Utafiti huu ulihusisha vigeu huru na vigeu tegemezi. Vigeu hivi ni muhimu katika utafiti wowote ule ambao unatarajia kuwa na matokeo ya kweli ambayo yanatumainiwa.Vigeu huru katika utafiti huu ni mikakati ya ufundishaji, vifaa vya ufundishaji, na kutathmini kazi ya wanafunzi. Hata hivyo vigeu huru huathiri vigeu tegemezi (Mugenda na Mugenda, 2003). Utafiti huu ulichunguza namna mikakati inayotumiwa katika ufundishaji huathiri umilisi wa usomaji wa fasihi ya watoto katika shule za msingi nchini Kenya. Kigeu tegemezi katika utafiti huu ni kimoja: umilisi wa usomaji. Katika muktadha wa umilisi huo wa usomaji, unaweza kuathiriwa na mikakati ya ufundishaji, vifaa vya ufundishaji, na kutathmini kazi ya wanafunzi.

## 3.4 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti ndogo ya Kasarani, Kaunti ya Nairobi, Kenya. Sababu za kuchagua wilaya hii ni kuwa matokeo ya mtihani wa (KCPE) yamekuwa hayaridhishi katika lugha ya Kiswahili kuanzia mwaka wa 2009 hadi 2012. Matokeo hayo yamekuwa katika kiwango cha chini ya ambayo ni chini ya asili mia hamsini. Sababu nyingine ni kwamba, wanafunzi wanaopatikana katika shule hizi wametoka katika jamii mbalimbali za kitabaka ambazo zina mapato tofauti tofauti. Kwa mfano, kuna wale ambao wazazi wao ni wenyemapato ya juu, ya wastani na yale ya chini. Jamii hizo zilizingatiwa kusaidia kuonyesha shule halisi za msingi nchini Kenya. Sababu nyingine ni kwamba, sehemu hii imepakana na Kauti ya Kiambu ambayo mazingira yake ni sawa na yale ya vijijini. Kuna

wanafunzi ambao hutoka kaunti ya Kiambu ili kuja kusomea katika baadhi ya shule zinazopatikana Kasarani. Kwa jumla,ilitarajiwa kuwa utafiti huu utatoa taswira ya wanafunzi wanaopatikana katika nchi nzima ya Kenya. Kwa sababu, kulikuwa na wanafunzi kutoka vijijini na mjini. Matokeo ya utafiti huu yalichukuliwa kama kiwakilishi cha shule zote nchini Kenya zinazofundisha fasihi ya Kiswahili katika shule za msingi.

### 3.5 Wasailiwa lengwa

Kaunti ndogo ya Kasarani ina shule ishirini na tano. Walimu waliolengwa ni wale tu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za umma. Madarasa yaliyolengwa ni ishirini na matano. Kadhalika, utafiti huu uliwalenga wanafunzi wa darasa la saba. Wanafunzi hao wa darasa la saba walichaguliwa kwa sababu wao wana ujuzi katika usomaji wa fasihi. Isitoshe,wanafunzi hao wamekuwa wakifundishwa fasihi ya Kiswahili tangu walipokuwa darasa la kwanza. Pia, wanaweza kuchukuliwa kuwa wana ujuzi zaidi wa kusoma vitabu vya fasihi. Kwa hivyo, walitarajiwa kuwa wana uwezo wa kuelewa wanayofundishwa na walimu wao.

Utafiti huu haukuzingatia madarasa ya chini-madarasa kuanzia la kwanza hadi la sita. Kwa mfano, wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la sita huwa bado hawana ujuzi wa usomaji wa vitabu hivyo hasa wanapolinganishwa na wale wa darasa la saba. Wanafunzi wa darasa la nane nao walitarajiwa kuwa na ujuzi zaidi ya wa darasa la saba lakini walitazamiwa kujitayarisha kufanya mtihani wa mwisho wa

kitaifa (KCPE). Vile vile, utafiti huu ulilenga sampuli ya walimu wanaofundisha Kiswahili darasa la saba katika shule hizoza msingi Kasarani. Walimu hao walikuwa wa muhimu katika utafiti huu.Kwa sababu, wao hutumia mikakati tofauti tofauti katika uelekezaji wa mafunzo ya wanafunzi katika kusoma fasihi ya Kiswahili ya watoto.

### 3.6 Sampuli na mchakato wa kuteua sampuli

Sampuli ziliteuliwa kwa kuzingatia mbinu makusudi katika kuchagua shule za serikali za msingi wilayani Kasarani. Mbinu hii ilitumiwa kwa sababu shule za kibinafsi hazikushirikishwa kwa sababu vitabu na vifaa vingi havifanani. Shule kumi na mbili ndizo zilizozingatiwa kutoka kwa maeneo mawili kutoka wilayani Kasarani. Makundi hayo mawili ni: shule zinazopatikana Kahawa na Ruaraka. Walimu waliteuliwa kwa kuzingatia mbinu maksudi kwa sababu ni walimu wanaofundisha Kiswahili katika darasa la saba. Hizi ni Shule za Umma katika Kaunti ndogo ya Kasarani kama inavyodhihirika katika Jedwali 3.1.

**Jedwali 3.1 Shule za kasarani zilizozingatiwa**

| Eneo | Shule za Msingi |
|---|---|
| Kahawa | Githurai |
| | Kahawa |
| | KU |
| | Roysambu |
| | Mahiga |
| | Kasarani |
| Ruaraka | Mathare |
| | Muthaiga |
| | GSU |
| | Baba dogo |
| | Drive-In |
| | Kariobangi North |

***Asilia:*** *Mkuu wa Elimu wa  ya Kasarani (2015)*

Baadhi ya shule zilizoteuliwa zimepakana na kaunti ya Kiambu. Ili kufikia idadi kusudia ya shule na walimu walioshiriki, walimu wa Kiswahili 12 katika darasa la saba waliteuliwa kimaksudi. Mtafiti pia alitumia njia ya nasibu kuteua wanafunzi 720 katika shule 12 za umma.Jedwali 3.2 linaonyesha uteuzi wa sampuli ya wasailiwa.

**Jedwali 3.2 Wasailiwa katika utafiti**

| Wasailiwa | Idadi Lengwa | Idadi iliyoteuliwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Walimu wa darasa la saba | 25 | 12 | 48% |
| Madarasa ya saba | 25 | 12 | 48% |
| Wanafunzi wa darasa la saba | 2400 | 720 | 30% |

***Asilia**: Mkuu wa Elimu wa Kasarani (2015)*

### 3.7 Njia na vifaa vya utafifi

Data ilikusanywa kwa kuzingatia vifaa vinne: Hojaji na mahojiano kwa walimu, kutazama somo linavyoendelezwa darasani na kutathmini insha za wanafunzi.Vifaa hivi vilitarajiwa kuwezesha kupata matokeo ambayo yalitegemewa katika utafiti huu. Hayo yameungwa mkono na Mugenda na Mugenda (2003) kwa kusisitiza kuwa, mtafiti akitumia vifaaa tofauti tofauti anatarajia matokeo ambayo yanaweza kutegemewa zaidi. Vifaa hivyo vilitumiwa kwa walimu na wanafunzi walioteuliwa.

#### 3.7.1 Maswali ya hojaji kwa walimu

Hojaji zilizotumiwa zilikuwa muhimu kwa ukusanyaji wa habari ambayo haiwezi kupatikana kwa kutazama tu au kwa mahojiano. Kutumia hojaji kulisaidia kupata hisia za watu, mielekeo yao na Tajiriba ya mtu binafsi (Gall, Borg na Gall, 1996). Hojaji hizo zilishirikisha maswali huru na funge. Hojaji hizo ziliwasilishwa kwa walimu kumi na wawili wa darasa la saba kutoka shule teule kumi na mbili.

Umuhimu wake ulikuwa ni kupata habari kamili kuhusu walimu wanaohusika, miaka yao, jinsia, ujuzi na viwango vyao vya elimu na mikakati ya ufundishaji wanayotumia.

### 3.7.2 Mahojiano

Mpangilio wa majadiliano ulitarajiwa kukusanya na kupata habari kutoka kwa walimu walioteuliwa. Majadiliano hayo yalitarajiwa kupata data ambayo ni vigumu kupata kupitia kwa hojaji. Data hiyo ilichangia ile ya hojaji. Mtafiti aliwasiliana na walimu wa darasa la saba kutoka shule zilizoteuliwa kupitia kwa njia ya mahojiano ili kupata habari kamili kuhusu mikakati na vifaa vinavyotumiwa.

### 3.7.3 Kuchunguza namna somo linavyofunzwa darasani

Njia hiyo ya utafiti ilitumiwa ili kutathmini mikakati inayotumiwa na walimu katika ufundishaji wa somo hili katika darasa la saba, usomaji wa vitabu mahususi vya fasihi ya watoto ya Kiswahili. Aidha, mafunzo hayo yalitazamwa kwa makini kwa kuzingatia namna walimu wanavyotumia vifaa katika ufundishaji na kuwashirikisha wanafunzi katika somo hili la fasihi ya watoto.

### 3.7.4 Kutathmini uhusiano wa fasihi ya watoto na kusoma

Kuchunguza kazi ya wanafunzi kulitoa matokeo halisi ya wanafunzi hao. Mtafiti angewafanya wanafunzi wawe na uoga kama angewapatia mtihani wafanye wangeweza wasifanye mtihani huo wakiwa katika hali yao waliyoizoea na mwalimu wao.

Mtafiti alichunguza insha ambazo zilikuwa zimeandikwa na wanafunzi vitabuni mwao. Mtafiti alizingatia kiwango cha msamiati kilichotumiwa; viakifishi vilivyotumiwa katika insha hizo; hali na kiwango cha kujieleza, mwandiko na alama alizopata mwanafunzi.

## 3.8 Majaribio ya vifaa vya utafiti

Kabla ya kutumia vifaa vya utafiti, majaribio ya nyanjani yalifanyiwa ili kuhakiksiha uhalali na ufaafu wavyo. Kwa kufanya hivyo shule za msingi za Kahawa Garisson na Thika Road ziliteuliwa. Ili kuhakikisha kuwa mbinu na vifaa vilivyotumika vilifaa. Vituo hivyo vilikuwa ni shule ambazo hazikuhusishwa moja kwa moja katika utafiti huu.  Pia, hojaji za walimu na mahojiano yalifanyiwa majaribio. Somo lilitazamwa darasani ili kupata uhalali na ufaafu huo. Vifaa vya utafiti ambavyo havikuwa vinaeleweka vilifanyiwa marekebisho yanayofaa.

### 3.8.1 Uhalali

Uhalali wa kifaa ni kipimo cha kuhakikisha ufaafu na utendakazi wake (Kombo na Troph, 2006). Uhalali wa vifaa hivyo ulipatikana katika shule za msingi za Kahawa Garisson na Thika Road ili kufanyiwa majaribio. Baadhi ya maswali ambayo hayakuwa yakieleweka yalifanyiwa marekebisho ya kadiri ili yaweze kusadifu katika upataji wa data zilizotarajiwa katika utafiti huu.

### 3.8.2 Utumainifu

Utumainifu kama kipimo cha viwango ambacho vifaa vya utafiti hutoa tathmini ya data ambayo hujaribiwa mara nyingi ili kutoa utumainifu (Mugenda na Mugenda,

2003). Majaribio hayo yalifanywa katika shule mbili teule. Shule hizo zilikuwa shule za msingi za Kahawa Garisson na Thika Road.

### 3.9 Ukusanyaji wa data

Katika maandalizi ya utafiti, mtafiti alipata hati rasmi ya kumtambulisha kwa shule alizofanyia utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta na nyingine kutoka Wizara ya Elimu. Baadaye mtafiti alizizuru shule hizo teule ili kupata kujifahamisha na kupata kibali kutoka kwa walimu wakuu. Mtafiti pia aliongea na walimu waliozingatiwa ili kuwaeleza azma yake ya kufanya utafiti uliotarajiwa. Aidha, aliwaelezea kuwa data zilizokusanywa zilihifadhiwa kwa siri. Mtafiti alizuru shule hizo kabla ya siku ya ukusanyaji wa data. Hili lilifanyika ilikuzoeana na kujenga mahusiano mazuri na walimu na wanafunzi kabla ya kuanza shughuli rasmi ya ukusanyaji wa data. Mpango huu ulisaidia katika kuandaa tarehe na kuwafunza wasailiwa. Mtafiti alikubaliana na walimu mada ya insha ili wanafunzi waandike kabla ya utafiti.

Siku ya kukusanya data, mtafiti alihakikisha kuwa ameketi nyuma ya darasa na kushuhudia namna walimu wanavyoendeleza somo hili la fasihi kwa wanafunzi wao. Kwa hivyo, mtafiti alipata fursa ya kutazama na kunakili yale yote yanayoendelea pale darasani. Baadaye mtafiti alimhoji mwalimu akitumia maswali teule yaliyoandaliwa kimbele kwa mahojiano. Vile vile, mtafiti alipanga na mwalimu kuhusu namna ya ujazaji wa hojaji. Mtafiti alipokea insha za wanafunzi ili kuzitathmini.

### 3.10 Uchanganuzi wa data

Data iliyotokana na vifaa vinne ilichanganuliwa kitadhania na kiidadi ili kubainisha ubora au udhaifu wavyo.Tarakilishi ilitumiwa katika kuchanganua asilimia na uwiano wa data zilizohusishwa baada ya uchanganuzi uliozingatia madhumni ya utafiti na mihimili ya nadharia. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kulingana na shule za Kasarani ambazo zimegawanyika katika sehemu mbili, Ruaraka na Kahawa. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo, majedwali na michoro mahususi.

### 3.11 Maadili katika utafiti

Mtafiti alizuru shule zilizofanyiwa utafiti na kujitambulisha kwa mwalimu mkuu na walimu.  Aliwaelezea azma yake ya kufanya utafiti. Aliwaelezea kuwa data na matokeo yalihifadhiwa kwa siri. Aidha, wasailiwa walifahamishwa kuwa matokeo hayo yalitumika tu kwa minajili ya utafiti unaokusudiwa. Isitoshe, watafitiwa walielezewa kimbele kuhusu umuhimu wa utafiti huu. Uzingativu huu ulijenga uaminifu na uwazi katika maelezo yanayotolewa. Kwa hivyo, utafiti huu ulitoa nafasi ya uhuru wa kushiriki kwa hiari bila ya kushurutuishwa kwa wasailiwa.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii iliwasilisha uchanganuzi wa data huku ikizingatia matokeo ya utafiti. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto na umilisi wa kusoma lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa darasa la saba. Takwimu za utafiti huu zilihesabiwa na kuchambuliwa kwa kutumia programu ya tarakilishi ya SPSS (Social Package for Social Sciences).

## 4.2 Demografia ya wahojiwa


Sehemu hii iliwakilisha sifa za kibinafsi za walioshirikishwa katika utafiti. Sifa hizi ziliwakilishwa kwa misingi ya jinsia, umri na kiwango cha elimu.

### 4.2.1 Usambazaji wa hojaji na mahojiano

Jumla ya hojaji 12 zilisambazwa wakati wa utafiti huu. Jumla ya walimu 12 pia walihojiwa ili kupata habari kuhusu mikakati inayotumiwa na walimu katika ufundishaji wa kusoma fasihi ya watoto. Mtafiti alichunguza shughuli za ufundishaji wa fasihi ya watoto katika shule 12 zilizoteuliwa kwa minajili ya uchanganuzi.

### 4.2.2 Jinsia ya walimu wa fasihi

Jinsia ya walimu kutoka shule zilizoshiriki katika utafiti imewakilishwa katika mchoro 4.1





**Mchoro 4. 1 Uwakilishaji wa walimu wa fasihi kijinsia**

Matokeo kuhusu jinsia ya walimu walikokuwa wanafundisha fasihi katika darasa la saba yanaonyesha ya kuwa, idadi kubwa (83%) ya walimu wa fasihi katika darasa la saba walikuwa wa jinsia ya kike ilhali wale wa jinsia ya kiume waliwakilishwa na asilimia 17. Matokeo haya yanaonyesha ya kwamba, kuna tofauti ya kijinsia inapokuja katika suala la kujiingiza katika shughuli za ufundishaji wa lugha katika shule za msingi. Hali hii iliweza kuhusishwa na desturi au imani ya kuwa, jinsia ya kike hufanya vyema sana katika masomo ya lugha (Babusa, 2010).

### 4.2.3 Umri wa walimu wa fasihi

Kubaini miaka ya walimu kumi na wawili waliotafitiwa, mchoro 4.2 uliwakilisha umri wao





**Mchoro 4.2 Uwakilishaji wa walimu wa fasihi kiumri**

Utafiti huu ulibaini ya kuwa (Mchoro 4.2) idadi kubwa (42%) ya walimu wa fasihi walikuwa kati ya miaka (31-40), waliokuwa na miaka kati ya (41-50) waliwakilishwa kwa asilimia 33 ilhali waliokuwa kati ya miaka (21-30) waliwakilishwa kwa asilimia 17. Hata hivyo walikuwa kati ya miaka 51-60 walikuwa na uwakilishi mdogo (kwa asilimia 8) katika utafiti huu. Kutokana na matokeo haya inaweza kudadisiwa ya kwamba idadi kubwa (asilimia 75) ya walimu wa fasihi katika shule za msingi walikuwa kati ya miaka (31-50), hali hii inaweza kuhusishwa na uzoefu wa miaka mingi katika shughuli ya ufundishaji ya fasihi ya watoto.

### 4.2.4 Kiwango cha elimu

Kiwango cha elimu cha walimu kutoka shule zilizoshiriki katika utafiti imewakilishwa katika mchoro 4.3




**Mchoro 4.3 Uwakilishaji wa walimu wa fasihi kulingana na kiwango cha elimu**


Utafiti huu ulibaini kiwango cha elimu cha walimu wa fasihi (Mchoro 4.3), asilimia 33 ya walioshiriki katika utafiti huu walikuwa na shahada ya vyuo vikuu, asilimia 17 walikuwa na vyeti vya diploma ilhali asilimia 50 walikuwa na vyeti vya ualimu. Ukizingatia matokeo haya ni dhahiri kuwa walimu wa fasihi katika shule za msingi wana elimu inayohitajika kuwawezesha kufunza fasihi ya watoto kwa ubora zaidi. Kwa hivyo, kiwango chao cha elimu hakiwezi kuwa kikwazo cha kuwafanya wasifunze fasihi ya watoto wakitumiwa mikakati itakayoleta mafanikio katika somo hili.  Utafiti unaonyesha ya kwamba muundo thabiti wa mafunzo ya walimu ni muhimu katika kukuza mageuzi katika mfumo. Kama inavyoweza kuthibitishwa katika uchunguzi wa Sifuna (1991) ni kwamba kutokufaulu kwa

mageuzi ya elimu hutokea kwa sababu ya mafunzo duni wanayopata walimu vyuoni kwani baadhi ya walimu hawapati mafunzo ya kufundisha fasihi ya watoto.

Utafiti huu ulibaini kiwango cha elimu cha walimu wa fasihi, asilimia 83.33(10) ya walioshiriki katika utafiti huu walikubali kuwa walisoma somo la fasihi kuwasaidia katika ufundishaji wao walipokuwa katika chuo cha ualimu. Hata hivyo, asilimia 17  hawakuwa na masomo mengine ya ziada.

### 4.2.5 Tajiriba katika ufundishaji wa Kiswahili

Walimu katika utafiti huu walikuwa wamefundisha kwa miaka tofauti. Kuna wale walikuwa wamefunza hata miaka hhadi ishirini. Miaka hii imewakilishwa katika mchoro 4.4.




**Mchoro 4.4 Tajiriba katika ufundishaji wa kiswahili**

Kutokana na utafiti huu,ilibainika kuwa walimu  waliokuwa na  Tajiriba ya miaka (11-15) walikuwa wengi (50%)  katika ufundishaji wa fasihi ilihali asilimia 17% ya walimu waliripotiwa kufunza kwa muda wa miaka kati ya sita na kumi

mtawaliwa. Data hii inaonyesha kuwa, licha ya idadi ya waalimu wanaofunza fasihi kuwa wengi, walio na Tajiriba ya ufundishaji wa Kiswahili kati ya miaka 11-15 ni wengi, masomo ya fasihi yamepata changamoto kutokana na mitaala ya kitambo. Kwa hivyo, mikakati mwafaka ya kutatua changamoto hizi ni kusajiliwa kwa mitaala mipya itakayo endeleza ufundishaji murua

### 4.2.6 Vipindi vya fasihi vilivyofunzwa kwa wiki

Walimu wote waliripoti kuwa kipindi kimoja pekee cha Kiswahili ndicho kilichotengwa kwa juma moja. Haya yanathibitisha kuwa Kiswahili hakijapewa muda wa kutosha. Ratiba za shule zinaporatibiwa, licha ya uzito wa mtaala wake.Ukosefu wa muda wa kutosha katika nyanja tofauti za ufunzaji umechangia pakubwa kwa matokeo duni. Kipindi kimoja kwa juma hakitoshi funzo la fasihi ya Kiswahili katika shule za msingi.

### 4.3 Mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya kiswahili

#### 4.3.1 Uzoefu wa kuendeleza mikakati ya ufunzaji wa fasihi ilivyoripotiwa na waalimu

Katika utafiti huu walimu walitumia mikakati tofauti katika ufundishaji wa somo la fasihi. Mikakati hii imewakilishwa ifuuatavyo katika jedwali 4.1.

**Jedwali 4.1 Ripoti ya walimu kuhusu mikakati waliyotumia**

| **Mikakati** | **Kila wakati** | | **Mara moja** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Idadi ya walimu** | **Asilimia (%)** | **Idadi ya walimu** | **Asilimia (%)** |
| Usomaji wa kipekee | 12 | 100.0 | 0 | 0 |
| Usomaji wa pamoja | 11 | 91.67 | 1 | 8.33 |
| Usomaji wa unachopenda | 4 | 33.33 | 8 | 66.67 |
| Usomaji wa kimya | 12 | 100.0 | 0 | 0 |
| Usomaji kwa sauti | 3 | 25.0 | 8 | 66.67 |
| Fasihi ya majadiliano | 4 | 44.33 | 8 | 66.67 |

Kutokana  na uchunguzi kutoka katika jedwali la kwanza, walimu wengi waliripoti kuwa usomaji wa kipekee na wa kimya ni moja wapo ya  mikakati  mikuu iliyotumiwa  kufunza fasihi katika shule za msingi kama ilivyo thibitishwa kwenye ripoti. Usomaji wa unachopenda, usomaji kwa sauti na fasihi ya majadiliano yapaswa kujumuishwa katika fasihi kila wakati ili kuboresha ukuzi wake.


Haya yalibainisha kuwa usomaji wa kimya na kipekee darasani mbinu mwafaka ya kufunza fasihi ilivyopendekezwa na waalimu. Utafiti ullibaini kuwa urahisi wa kijisomea kwa wanafunzi ulionekana maarufu kwa waalimu wengi.

Usomaji kwa sauti kama mbinu ya kufunza fasihi unatumiwa mara moja tu. Matokeo haya yanaweza kufananishwa na yale ya mwandishi Camber (1980) alipokiri kuwa mikakati ya kusoma kwa sauti na usimuliaji wa hadithi ndizo mbinu mwafaka zinazotakikana kutumiwa shuleni, kwa kuwa huibua hamu ya wanafunza kusoma. Haya yaweza kuchangia matumizi ya mbinu hizi kwa wingi pindi zinapojumuishwa. Kwa kuzingatia ujuzi wa waandishi mbalimbali. Waalimu huchukulia vigezo vyao kama vya upeo wa juu, visivyo kuwa kiwango cha wanafunzi wa madarasa ya msingi.

Usomaji wa kipekee na usomaji wa kimya ulionekana kama mojawapo ya mbinu za kufunza fasihi madarasani. Haya yanatokana kwa urahisi wa kujumuisha mbinu hizi katika mazingira ya darasani, kwani katika mikakati hii walimu huwacha wanafunzi kusoma bila kuwaelekeza. Baadhi ya matukio katika fasihi hujikita katika fasihi ya mazungumzo. Sababu zikiwa kuwa fasihi hii hutumia Kiswahili katika uwasilishaji. Baadhi ya walimu wamekuwa wakikashifiwa kwa kutumia mbinu moja ya ufundishaji mwaka baada ya mwaka licha ya mabadiliko katika sekta ya teknolojia kwa kuwa wanakisia kuwa enzi za zama.

### 4.3.2 Njia zinazowavutia wanafunzi nyakati za mafunzo ilivyripotiwa na waalimu

Wanafunzi walipokuwa wakisoma kuna zile njia za ufundishaji ambazo ziliwavutia zaidi. Njia hizo zimewakilishwa katika mchoro 4.5





**Mchoro 4.5 Njia zinazowavutia wanafunzi nyakati za mafunzo ilivyripotiwa na walimu**

Kutokana maoni ya waliohojiwa, idadi kubwa ya walimu walioshiriki katika mahojiano walieleza kuwa walimu hupendelea kusoma kwa kimya na kipekee. Wanafunzi hupendelea mikakati ambayo walimu hawatumii kila wakati wanaposoma fasihi. Hata hivyo, kusoma kwa pamoja ilikisiwa kama njia isiyokuwa mwafaka zaidi na isiyopendeza wengi wa wanafunzi. Kwa hivyo, kuna uwezekano wa kujumuishwa kwa njia hii ili kufudisha fasihi licha ya kutopendwa na wanafunzi wengi.

### 4.3.3 Changamoto za ufundishaji wa fasihi ya watoto darasani

Walimu waliulizwa maswali kuhusu changamoto waliozikumbana nazo katika ufundishaji wa fasihi katika darasani. Mchoro 4.6 unaonyesha matokeo haya.




**Mchoro 4.6 Ripoti ya walimu kuhusu changamoto za ufundishaji wa fasihi**

Kulingana na matokeo ya utafiti uliofanywa (Mchoro 4.6) ilibainiwa kuwa mikakati isiyofaa ilikuwa changamoto kuu kwenye ufundishaji wa fasihi katika darasa la saba ilivyoripotiwa na idadi kubwa (asilimia 42) ya walimu. Kama inavyoweza kudhibitishwa na uchunguzi wa Ngugi (2009), hata kama mitaala na vifaa vimepangwa vizuri na walimu hawajapatiwa mafunzo yakutosha madhumuni ya mitaala hiyo hayatatimizwa. Changamoto nyingine zilizoripotiwa na walimu ni kama idadi ya wanafunzi darasani, kitabu kinachosomwa darasani na muda mfupi kwa kusoma kitabu za hadithi.

Kutokana na matokeo ya kutazama somo darasani, ilikisiwa kuwa asilimia 83.3 ya walimu walifanya matayarisho ya ratiba zao za mitaala ya Kiswahili ilhali 16.67%

miongoni mwao hawakufanya matayarisho yoyote. Asilimia 50 ya walimu walifanya matayarisho ya kipindi ilhali waliosalia hawakuzingatia kufanya matayarisho ya kipindi.Kiwango cha ufunzaji darasani kiliwakilishwa kwa Jedwali 4.2.

**Jedwali 4.2 Kiwango cha Kujitayarisha cha Walimu Waliotumia Mitaala ya Somo la Fasihi**

| Ujuzi | Idadi ya walimu | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Mzuri zaidi | 1 | 8.33 |
| Mzuri | 2 | 16.67 |
| Wastani | 6 | 50.0 |
| Usioridhisha | 2 | 16.67 |

## 4.4 Baadhi ya vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wa fasihi katika shule za msingi

Vifaa katika ufundishaji wa fasihi ni muhimu. Vifaa hivi vinapotumiwa vilivyo huwafanya wanafunzi kuelewa wanachofunzwa na kufurahia somo la fasihi. Walimu katika shule zilizoshirikishwa katika utafiti hutumia vifaa tofauti kama inavyoonyesha katika jedwali 4.3.

**Jedwali 4.3 Uzoefu wa vifaa vya ufundishaji wa fasihi vilivyotumiwa katika shule za msingi**


| Vifaa | Kila Wakati | | Mara Mojamoja | | Havitumiki | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Radio | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 100 |
| Ubao | 12 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Runinga | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 100 |
| Filamu | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 100 |
| Magazeti | 0 | 0 | 6 | 50 | 6 | 50 |
| Vitabu vya hadithi | 12 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Picha | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 100 |
| Vinasa sauti | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 100 |
| Mabango | 8 | 66.67 | 4 | 33.33 | 0 | 0 |

Kulingana na matokeo ya utafiti uliofanywa, asilimia mia moja ya waliohojiwa walikubali kutumia zaidi vitabu vya hadithi vilitumiwa na ubao ndio uliotumiwa nyakati za mafunzo ya fasihhi. Hatahivyo, vifaa vya teknolojia ya kisasa kama vile redio,runinga, filamu na vinasa sauti havikutumiwa kamwe. Kwa hivyo, ni thibitisho tosha kuwa vitabu vya hadithi ndivyo vilivyotumiwa kwa wingi katika

ufunzaji wa fasihi. Haya pia yanaonyesha kuwa, walimu wengi wana dhana ya uasilia kuwa vitabu vya hadithi ndivyo vinaweza kuwa na uwasilishaji murua wa fasihi.

### 4.4.1 Changamoto ya uteuzi wa vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wa fasihi ya watoto

Vifaa vya ufundishaji vinapoteuliwa ili vitumiwe katika ufundishaji wa fasihi huwa kuna changamoto. Changamoto hizi zimewakilishwa katika mchoro 4.7.




**Mchoro 4.7 Changamoto ya uteuzi wa vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wa fasihi ya watoto ilivyoripotiwa na walimu**


Matokeo ya Mchoro4.7 yalionyesha kuwa bei ghali ya vifaa vya kusomesha fasihi ilikuwa changamoto katika ufundishaji ilivyoripotiwa na idadi kubwa ambayo ni asilimia 67 ya walimu. Haya yaonyesha kuwa shule zinahitaji mikakati mwafaka katika bajeti ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujumuishwa kwa

matokeokabambe ya fasihi. Changamoto zingine zilizoripotiwa ni ukosefu wa rasilmali kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na shule za msingi kwa sababu ya elimu ya bure.

Kutokana na matokeo katika mahojiano na walimu wa kiswahili darasa la saba, walimu watano waliripoti kuwa walitumia vifaa zaidi ya moja katika ufundishaji wao. Vilevile, walimu wanane waliripoti wanafunzi hawaelewi wanachokisoma kwa urahisi, walimu wao walipotumia vifaa katika ufundishaji wa kusoma fasihi. Matokeo pia yalionyesha kuwa walimu wote walikubali kuwa wanafunzi walijihusisha na kujibu maswali walipofundishwa. Walimu wanane waliripoti kuwa kujadiliana ni mmoja wapo ya mbinu inayotumiwa katika fasihi ilhali walimu wanne waliripoti kuigiza kama mbinu mbadala. Hata hivyo, hakuna aliyeripoti matumizi ya kuandika na kueleza kwa mukhtasari wakati wa kufundisha. Walimu wote walikubali ya kwamba shughuli hizo za wanafunzi huwasaidia katika usomaji.

### 4.4.2 Jinsi wanafunzi walivyopewa zoezi la kusoma

Mazoezi katika somo la fasihi ni muhimu ili kuweza kutathmini somo. Mchoro 4.8 unaonyesha matokeo haya.




**Mchoro 4.8 Jinsi wanafunzi walivyopewa zoezi la kusoma**

Kutokana na matokeo ya Mchoro 4.8, ni dhahiri kuwa idadi kubwa (92%) ya walimu waliripoti kuwa wanafunzi walipewa zoezi la kusoma mara moja tu kwa wiki. Hata hivyo, asilimia 8 ya walimu waliripoti kuwa wanafunzi hawakupewa mazoezi ya kusoma jinsi itakikanavyo katika fasihi.


Hii inaashiria kuwa, walimu wengi hawatili maanani kazi ya fasihi. Kwani walimu hawakujishughulisha katika kujenga mwelekeo ufaao katika hali ya usomaji. Odaga (1985), ameshughulikia suala la ufundishaji wa fasihi na amefafanua kwamba, mchango wa walimu ni muhimu katika ufundishaji wa fasihi ya vijana.

Amekariri kuwa, walimu na shule wajishughulishe kwanza katika kujenga mwelekeo ufaao ndipo kutakuwa na mabadiliko katika hali ya usomaji.

Kutokana na matokeo katika mahojiano na walimu wa kiswahili darasa la saba, idadi kubwa (100%) ya walimu waliripoti kuwa lugha za Kiswahili na Kiingerezazilitumiwa miongoni mwa wanafunzi wa darasala la kwanza hadi la nane.Walimu waliripoti kuwa lugha hizo mbili zilikuwa na manufaa zaidi katika kuimarisha kiwango cha usomaji wa vitabu vya hadithi shuleni, kwa mfano wanafunzi huweza kujieleza vizuri na kufahamu kusoma.

### 4.4.3 Ushiriki wa walimu wa fasihi katika kuwachagulia wanafunzi vitabu vinavyotumiwa shuleni

Katika utafiti huu walimu wengine walishiriki katika kuwachagulia wanafunzi vitabu na wengine hawakushiriki. Mchoro 4.9 umewakilishwa ushiriki huu.




**Mchoro 4.9 Wanaojumishwa kuwachagulia wanafunzi vitabu vinavyotumiwa shuleni**

Matokeo kutoka kwenye Mchoro 4.9 inaonyesha kuwa baadhi ya walimu waliojibu swala la ushirikiano katika kumchagulia mwanafunzi kitabu cha kusoma, asilimia 75 walisema hawashiriki na asilimia 25 pekee walisema wanashirika. Haya yaliashiria kuwa waalimu hawakujumuishwa katika kuchaguliwa wanafunzi vitabu vya hadithi ya fasihi miongoni mwa wanafunzu. Odaga (1985), ameshughulikia suala la ufundishaji wa fasihi na amefafanua kwamba, mchango wa walimu ni muhimu katika ufundishaji wa fasihi ya vijana. Walimu wanahitaji kushirikishiwa katika kuwachagulia wanafunzi vitabu.

**Jedwali 4.4 Ripoti ya walimu kuhusu uchaguzi wa vitabu shuleni**

| Jinsi ya kuchagua vitabu shuleni | Idadi ya walimu | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Taasisi ya elimu | 8 | 66.67 |
| Mwalimu mkuu | 4 | 33.33 |
| Wazazi | 0 | 0 |
| Mwalimu wa darasa | 7 | 58.33 |

Kutokana na matokeo katika Jedwali 4.13, idadi kubwa 8(asilimia 66.67) waliripoti kuwa vitabu vilivyotumiwa shuleni vilikuwa vikichaguliwa na taasisi ya elimu. Wakati mwingine walimu wakuu na walimu wasimamizi wa madarasa ndio waliohusika kuchagua vitabu vilivyotakiwa kutumiwa na wanafunzi. Iliripotiwa kuwa shule zilizo na maktaba zingewatumia walimu kutathmini idadi ya vitabu vitakavyokidhi mahitaji ya wanafunzi.

**Jedwali 4.5 Idadi ya vitabu kwenye maktaba**

| Idadi ya vitabu kwenye maktaba | Idadi ya walimu | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| 1-20 | 2 | 16.67 |
| 21-40 | 7 | 58.33 |
| Zaidi ya 41 | 3 | 25 |

Kutokana na ripoti katika Jedwali 4.5, idadi kubwa (asilimia 58.33) ya walimu waliripoti kuwa walikuwa na vitabu kati ya ishirini na moja hadiarubaini. Hata hivyo, kiwango hiki cha vitabu hakitosherezi wanafunzi shule iliyokuwa na zaidi ya vitabu arobainina kimoja. Wanafunzi wanahitaji vitabu vingi katika maktaba ili wavisome.

Kutokana na data iliyochukuliwa walimu wakifunza, ilingamuliwa kuwa idadi kubwa ya walimu walikuwa wakitumia vifaa kama ubao na vitabu vya hadithi katika ufundishaji wao. Kwa kutumia vifaa hivyo, walimu walitathminiwa na kutuzwa alama zifuatavyo.

**Jedwali 4.6 Jinsi ya kutumia ubao kufundisha fasihi**

| Jinsi ya kutumia | Idadi ya walimu | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Vizuri zaidi | 2 | 16.67 |
| Vizuri | 4 | 33.33 |
| Wastani | 5 | 41.67 |
| Isiyoridhisha | 1 | 8.33 |

Ilibainika kuwa, wengi wa walimu (asilimia 41.67) wa fasihi walitumia ubao kufunza fasihi. Ingawaje, idadi ndogo ya walimu (16.67%) wa fasihi walitumia ubao vizuri zaidi. Hii ni ishara kuwa kufunza fasihi madarasani hakukuzingatia ili vilivyo, kuvuta mtazamo wa wanafunzi waliohudhuria vipindi vya fasihi.

### 4.5 Umilisi wa kusoma fasihi miongoni mwa wanafunzi

Umilisi wa kusoma Fasihi miongoni mwa wanafunzi ulitathminiwa kwa kuzingatia umaarufu na ubingwa wa wanafunzi wa kuandika Insha kwa kuzingatia vigezo vya sarufi kama vile; uakifishaji, tahajia, msamiati, uwasilishaji wa ujumbe na mpangilio na mtindo. Matokeo haya yaliwasilishwa ifuatavyo:

**Jedwali 4.7 Alama za wanafunzi za insha zilizotathminiwa**

| | Alama alizotuzwa | Uakifishaji | Tahajia | Msamiati | Uwasilishaji wa ujumbe | Mpangilio na mtindo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama za juu | 40 | 3 | 3 | 12 | 14 | 8 |
| Alama wastani | 17.07 | 0.71 | 0.77 | 4.80 | 7.08 | 3.72 |
| Alama katika sehemu (%) | 42.68 | 23.70 | 25.56 | 39.98 | 50.56 | 46.49 |

Insha zilituzwa alama ya juu ikiwa 40. Alama za wastani walizotuzwa wanafunzi zikiwa 17.07 hizi zikifananishwa na asilimia 42.68 kwa wanafunzi. Haya yaliashiria kuwa kati ya sehemu tano zilizotuzwa, wanafunzi walifanya wastani sehemu ya uwasilishaji wa ujumbe. Hata hivyo, wanafunzi wengi hawakufanya vyema katika tahajia. Alama katika uakifishaji, msamiati na mpangilio na mtindo zilionekana kuwa chini ya wastani. Kwa sababu, baadhi ya vipera vya fasihi simulizi havikushughulikiwa na walimu wa fasihi walipokuwa wakifundisha fasihi ya watoto. Gituku (1990), ameshughulikia vipera vya fasihi simulizi. Amechunguza namna vipengele vya ufundishaji wa kimawasiliano kutoka katika maigizo ya watoto ya kienyeji kama njia inayofanya ufundishaji wao katika shule za msingi.

**Jedwali 4.8 Utuzaji wa alama kwenye insha**

| Jamii ya alama (x/40) | Idadi ya wanafunzi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| 1 – 10 | 102 | 14 |
| 11 – 20 | 426 | 59 |
| 21 – 30 | 192 | 27 |
| 31 – 40 | 0 | 0 |
| Jumla | **720** | **100** |

Wanafunzi wengi (asilimia 59) walituzwa alama kati ya 11 na 20 juu ya alama 40. Asilimia 73 ya wanafunzi walipata alama chini ya alama 20 juu ya 40.

**Jedwali 4.9 Kutuzwa kwa alama kwa kuzingatia sehemu ya uakifishaji na tahajia**

| Alama | Uakifishaji (3) | | Tahajia (3) | |
|---|---|---|---|---|
| | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** |
| 0 | 300 | 41.67 | 274 | 38.06 |
| 1 | 328 | 45.56 | 340 | 47.22 |
| 2 | 92 | 12.78 | 106 | 14.72 |
| 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |

Kutokana na matokeo katika Jedwali4.18, matokeo katika Uakifishaji na Tahajia yalikuwa mabaya.

**Jedwali 4.10 Alama kwa kuzingatia sehemu ya msamiati, uwasilishaji wa ujumbe na mpangilio na mtindo**

| Jamii ya alama (x/40) | Msamiati (12) | | Uwasilishaji wa ujumbe (14) | | Mpangilio na mtindo (8) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| 1 - 3 | 190 | 26.39 | 34 | 4.72 | 128 | 17.50 |
| 4 - 6 | 378 | 52.50 | 360 | 50.00 | 396 | 55.00 |
| 7 - 9 | 150 | 20.83 | 324 | 45.00 | 192 | 26.67 |
| 10 - 12 | 2 | 0.28 | 2 | 0.28 | 6 | 0.83 |

Matokeo yalibainisha kuwa wanafunzi walifanya vyema katika Uwasilishaji wa ujumbe katika insha zao jinsi ilivyoripotiwa na walimu, wanafunzi (asilimia 45) walipata alama kati ya 7 na 9. Hata hivyo, wanafunzi wengi walifanya kazi yao wastani katika msamiati, mpangilio na mtindo.

Kwa hivyo, kuna haja ya walimu wanaofunza kusoma fasihi wazingatie uwezo wa wanafunzi kuelewa vyema vipengele vya fasihi ili wawe wenye faida katika jamii. Isitoshe, ni jukumu la mwalimu kumfanya mwanafunzi wake awe bora kwa kupata alama za juu katika mtihani wake na aweze kuyaambatanisha na mazingira yake. Kwa hivyo, mwanafunzi awe na ujuzi wa kulongea lugha na kuitumia vipasavyo anapoasiliana. Kutofunza kwa fasihi shuleni ingekuwa kama kizuizi cha kuleta mafanikio ya kuendeleza mitaala ya fasihi. Kwa hivyo, fasihi hukumbwa na changamoto kuu kama vile ukosefu wa vifaa mwafaka katika shule za upili na msingi.

Uchunguzi miongoni mwa shule bora za msingi nchini Kenya na kudhibitishwa kuwa kulikuwa na uhaba wa vitabu vya hadithi ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wanavivyotumia. Kitabu kimoja cha kiada kilionekana kutumiwa na wanafunzi kati ya watatu na wane.  Uchunguzi huo pia ulionyesha kuwa vitabu vya Kenya Institute of Curriculum Development (KICD) havikuepo na ambapo vilikuepo havikutumia vyema na walimu.

Uchunguzi uliofanywa na Ipara (2004) ni kwamba, mmoja wapo mwalimu wa Kiswahili kutoka jimbo moja nchini Kenya, alibaini kuwa baadhi ya vitabu vinavyotumiwa vilikuwa na mpangilio rahisi unaokidhi mahitaji ya kiwango fulani cha wanafunzi. Licha ya uchunguzi huo, Bennars na wengine (1994) walibaini kuwa vifaa vya mwongozo vilikuwa muhimu kwa ufundishaji wa somo lolote.

Siku hizi kuna uimarishaji wa maendeleo katika vifaa vya miongozo inayotokana na kuimarisha teknolojia. Walimu huchagua mbinu mwafaka ya kuwasilisha vifaa vya miongozo kuzingatia vigezo vinavyoweza kusaidia kulenga kusudi la miongozo hiyo (Mukwa, 1988).

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha ufupisho wa matokeo, hitimisho na mapendekezo katika uchanganganuzi.

## 5.2 Muhtasari

Sehemu hii yailenga kuelezea matokeo ya mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili katika shule za msingi Kasarani. Vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji na umilisi wa kusoma miongoni mwa wanafunzi.

### 5.2.1 Mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya kiswahili

Kutokana  na uchunguzi walimu wengi waliripoti kuwa usomaji wa kimya na wa kipekee ni moja wapo ya  mikakati  mikuu iliyotumiwa  kufunza fasihhi katika shule za msingi kama ilivyo thibitishwa kwenye ripoti. Usomaji wa unachopenda, usomaji kwa sauti na fasihi ya mzunguko yapaswa kujumuishwa katika kusoma fasihi ili kuboresha  ukuzi wake. Kutokana na maoni ya waliohojiwa, asilimia 100% ya walimu walioshiriki katika mahojiano walieleza kusoma  kwa sauti ndio husaidia wanafunzi katika umilisi wa kusoma. Hata hivyo, kusoma kwa pamoja, kimya na kipekee, ilikisiwa kama njia zisiyokuwa mwafaka na zisizowapendeza wengi wa wanafunzi, kwa hivyo kuna uwezekano kujumuishwa kwa njia hizi kwa njia ifaayo ilikufudisha fasihi licha ya kutopendwa na wengi wa wanafunzi.

Hata hivyo walimu hawa walisema kuwa, kusoma kwa sauti husaidia katika umilisi wa lugha na asilimia kubwa hawatumii mikakati hii katika ufundishaji. Mikakati inayotumiwa na walimu katika ripoti haiwavutii wanafunzi.

### 5.2.2 Baadhi ya vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wa fasihi katika shule za msingi

Kulingana na matokeo ya utafiti uliofanywa, asilimia mia moja ya waliohojiwa walikubali kuwa matumizi ya vitabu vya hadithi vilikuwepo na ubao ndio uliotumiwa nyakati za mafunzo ya fasihi. Hata hivyo, vifaa vya technolojia ya kisasa kama vile redio, runinga, filamu na vinasa sauti havikutumiwa kamwe. Kutokana na matokeo katika mahojiano na walimu wa kiswahili darasa la saba, (asilimia 40) waliripoti kuwa walitumia vifaa zaidi ya kimoja katika ufundishaji wao. Asilimia 60 hawakutimia vifaa zaidi ya kimoja.

Ilibainika kuwa wengi wa walimu (asilimia 41.67) wa fasihi walitumia ubao kufunza fasihi. Ingawaje, ni idadi ndogo ya walimu (16.67%) wa fasihi waliotumia ubao vizuri zaidi. Hii ni ishara kuwa kufunza kwa fasihi madarasani hakuzingatiwi vilivyo, ili kuvuta mtazamo wa wanafunzi waliopohudhuria vipindi vya fasihi.

### 5.2.3 Umilisi wa kusoma fasihi miongoni mwa wanafunzi

Insha zilituzwa alama za juu zikiwa 40. Alama za wastani walizotuzwa wanafunzi zikiwa 17.07. Haya yaliashiria kuwa kati ya sehemu tano, wanafunzi walifanya wastani sehemu ya uwasilishaji wa ujumbe. Hata hivyo, wanafunzi wengi hawakufanya vyema katika tahajia. Vile vile, alama katika uakifishaji, msamiati

na mpangilio na mtindo ulionekana kuwa chini ya wastani. Kwa sababu, baadhi ya vipera vya fasishi simulizi havikushughulikiwa na walimu wa fasihi walipokuwa wakifundisha fasihi ya watoto. Matokeo yalibainisha kuwa wanafunzi walifanya vyema katika Uwasilishaji wa ujumbe katika insha zao jinsi ilivyoripotiwa na walimu, wanafunzi 324 walipata alama kati ya 7 na 9.

Kwa hivyo, kuna haja ya walimu wanaofunza fasihi wazingatie mikakati mwafaka katika ufundishaji wa fasihi ili wanafunzi waelewe vyema vipengele vya fasihi ili wafaidike katika umulisi wa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, ni jukumu la mwalimu kumfanya mwanafunzi wake awe bora kwa kupata alama za juu katika mtihani wake na aweze kuyaambatanisha na mazingira yake. Kwa hivyo, mwanafunzi awe na ujuzi wa kulonga na kutumia ipasavyo lugha anaposoma na kufanya mtihani katika lugha ya Kiswahi.

### 5.3 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti, walimu wote (ambapo ni asilimia mia moja) waliripoti kuwa usomaji wa kimya na kipekee ni mikakati mikuu iliyotumiwa kufunza fasihi katika shule za msingi. Mikakati kama vile, usomaji wa unachopenda, usomaji wa kipekee, usomaji kwa sauti na fasihi ya mazunguko haikujumuishwa katika fasihi kila wakati. Sababu zikiwa ni kwamba mikakati hii inahitaji mwalimu kuwaelekeza wanafunzi kusoma. Walimu wa fasihi katika utafiti hupendelea kuwapatia wanafunzi vitabu wajisomee.

Asilimia kubwa ya walimu hawaelekezi wanafunzi. Wanafunzi wanapatiwa vitabu na wanaambiwa wajisomee wenyewe. Kulingana na matokeo makuu ya uchunguzi

huu, wengi wa walimu walihojiwa walikubali kuwa vitabu vya kiada vinavyotumiwa na wanafunzi havitoshi na ubao ndio ulitumiwa kwa wingi nyakati za mafunzo. Hata hivyo, vifaa vya kisasa kama redio, runinga, filamu, vinasa sauiti havikutumiwa. Ni bayana kwamba, vitabu vya hadithi vinavyotumiwa darasani ni vichache.

Katika kutazama somo darasani walimu wengi hawakuwa wametayarisha mwongozo wa kufundisha somo la kusoma fasihi. Hii iliwafanya wasifunze kwa utaratibu unaokubalika.

Ilibainika kwamba kati ya sehemu tano, wengi ya wanafunzi walifeli kwenye sehemu ya tahajia.  Mbali na hayo, alama katika uakifishaji, msamiati na mpangilia na mtindo ulikuwa chini ya wastani. Miongozo ya kupasha ujumbe husaidia kuongeza dhana ya ukweli kama vile picha. Kwa hivyo, kuna haja ya uangalifu unapochagua vitabu vya kusoma fasihi kuhakikisha kwamba vinafaa katika mafunzo ya fasihi kwenye viwango tofauti vya elimu.

## 5.4 Mapendekezo ya utafiti

### 5.4.1 Mapendekezo kwa walimu na Wizara ya Elimu

Mapendekezo yafuatayo yalifanywa.

1. Walimu wanafaa watumie mikakati tofauti tofauti kila wakati si kupendelea mikakati mingine zaidi ya mingine. Walimu wazingatie mikakati inayopendelewa na wanafunzi. Mikakati kama vile kusoma kimya huwafanya wanafunzi wasipate motisha ya kusoma kwa mfano, kama mwanafunzi hana

uraibu wa kujisomea. Walimu wawashughulishe wanafunzi zaidi katika somo wanapofundisha.

2. Kwa kiwango kikubwa kusoma fasihi hakukuimarishwa na kupewa kipao mbele, Kwani, vipindi cha somo hili ni kimoja tu kati ya vipindi vitano. Vifaa vikuu kama vitabu maalum vya fasihi, vifaa vya kisasa kama radio, runinga, filamu, vinasa sauti na vifaa vyovyote vya teknolojia ya kisasa havikutumiwa. Hivi vifaa vinasaidia sana kuimarisha akili ya mtoto kisaikolojia, kijamii na pia kuibulia fikira ya uelewa wa dunia wanamoishi. Kwa hivyo, wizara ya elimu inafaa ishughulikie vifaa hivyo kwa njia ya usawa katika shule za msingi nchini Kenya ili kumairisha na kutekeleza masomo ya fasihi.

3. Ilibainika kwamba, wanafunzi wengi hawafanyi vizuri katika kila sehemu ya kuandika insha katika shule za msingi. Ili kuendeleza masomo ya fasihi na kufaulu kwa ukamilifu, ni jukumu la walimu kutenga mikakati inayowafaa ambayo itaboresha masomo ya fasihi kwa kiwango cha juu.

4. Wanafunzi wahimizwe kusoma vitabu vya kutosha. Wasome magazeti ya Kiswahili na majarida; hii itasaidia kuimarisha lugha ya Kiswahili. Walimu pia wapangiwe warsha na semina za kuwafunza kufundisha fasihi ya watoto ya Kiswahili. Walimu wahimizwe kutayarisha somo kabla ya kufunza.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa utafiti zaidi

1. Utafiti ufanywe kuhusu changamoto zinazotokana na vitabu vichache vya hadithi katika maktaba za shule za msingi

2. Kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu namna vifaa vya kiteknolojia ya kisasa vinaweza kutumiwa na walimu wa shule za msingi katika ufundishaji wa fasihi ya watoto.

3. Utafiti zaidi unaweza kufanywa katika kaunti zingine zilizopo nchini Kenya. Tafiti hizo zinaweza kuwa sawa na huu lakini ziwe zinalinganisha zaidi jinsi ufundshai unavyotekelezwa na walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili na fasihi kwa wanafunzi wa shule za msingi.

## MAREJELEO


Ahmad, F. & Aziz, J. (2009). Students' Perceptions of the Teachers of Literature Communicating and Understanding Through the Eye of Audience. European. *Journal of Social Sciences*, 7 (3) 17. Retrieved from: www. eujournal.com/ejss7302.pdf on 12/3/2012.

Akoleit, J. (1990). "Response and Criticism in Children's Literature in Kenya: The Case of Barbara Kimenye". Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Alembi, E. (1992). "An Analysis of Style and Social Significance of the Abanyole Children's Oral Poetry". Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Alembi, E. (2007). *Phases and Dynamics in Children's Literature in Kenya. In the 10th Nairobi Book Fair, Booklet.* Nairobi: Kenya Publishers Association.

Allan, D. (1973). *Literature for Children. London*: Eyre and Spottiwood Ltd.

Arbothnot, M. & Sutherland, Z. (1972): *Children's Literature*. London: Scott Forsman and Company.

Ayot, H. O. & Olembo, J. O. (eds) (1986). *Seminar on Evaluation of Material Developed for B.Ed (Primary).* A Report of a Seminar held at Mosoriot Teacher's College 2 – 21, January 1986. Nairobi. Kenyatta University Faculty of Education and University of London Institute of Education.

Babusa, O.H. (2010). "Uchanganuzi linganuzi wa mielekeo na umilisi wa lugha ya Kiswahili wa wanafunzi katika mikoa ya Pwani na Nairobi nchini Kenya". Tusnifu uzanifu, *Chuo Kikuu cha Kenyatta* (Haijachapishwa).

Bennars, G. A., Otende, J. E., & Boisevert, B. R. (1994). *Theory and Practice of Education.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Benton, M. & Fox, G. (1985). *Teaching Literature Nine to Fourteen*. New York.: Oxford University Press.

Bindra, S. (2007). *Why Kenyans are not Reading*, Sunday Nation, August 26, 2007. Nairobi.

Brooks, E. (1982). *Language and Thinking in School*. New York: Rinehart and Winston.

Bukenya, R. C., Buss, R. R., Stanley, W. B., Blanchard-Fields, F., Cho, J. R., na Druhan, B. (1996). The role of implicit and explicit processes in learning from examples: A synergistic effect. *Journal of Experimental Psychology: Learning, Memory, and Cognition*, 15, 1083-1100.

Cass, J. (1967). *Literature and Young Children*. London: Longman Group Ltd.

Chacha, L. M. & Musau, P.M. (2001). *Mbinu za Kisasa za Kufundisha Kiswahili kwa Walimu wa Shule za Msingi, Upili na Vyuo*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Chakava, H. (1994). *Books and Reading in Kenya*. In Studies on Books and Reading No. 3. UNESCO.

Chang, W. (2002). *The Impact of Constructivist Teaching on Students' Perceptions on Teaching and Learning*. Paper Presented at the Annual Meeting of the National Association for Research om Science Teaching. New Orleans. L. A.

Chang, Y. (2010). *Students' Perceptions of Teaching Styles and Use of Learning Strategies*. Retrieve from http.//trace.tennessee.edu/ukgradthes/782 on 27/8/2012

Collie, J. & Slater, S. (2000). *Literature in the Language Classroom: A Resource Book of Ideas and Activities*. United Kingdom: Cambridge University.

Combes, H. (1953). *Literature and Criticism*. London: Penguin Books.

Commeyras, M. & Inyega, H. (2007). *An Integrative Review of Teaching in Reading in Kenyan Primary Schools*. Reading Research Quarterly 42(2) 258-281.

Davies, A. (1973). *Literature for Children*. Oxford: The Open University Press.

Dike, V. W. (1995). *Literary without Libraries: Promoting Literacy Among School Children in Nigeria*. Traditional Cultural and Technological. Selected Papers from 23rd Annually Conference of International Association of School Librarianship. Pittburg.

Dires, A. (2008). "The Use of Children's Literature in Second Cycle Primary School". Tasnifu ya M.A. Addis Ababa University. (Haijachapishwa).

Flavia, A. T. (2011). Children's Literature in African Language Swahili for Children in Kenya and Tanzania. *A Journal University of Calabria*.

Fox, G. (1996). *Teaching Fiction and Poetry, in International Comparison Encyclopedia of Children's Literature*. New York: Routledge.

Gachukia, E. & Akivaga, S. K. (eds) (1978). *Teaching of African Literature in Schools.* Nairobi: KLB.

Gall, M.; Borg, W. & Gall, J. (1960). *Educational Research: An Introduction* (6th Ed). New York: Longman.

Ghosn, I.K. (2003). *Socially Responsible Language Teaching Using Literature in the Language Teacher*. Retrived from: http//www.jalt-publications.org/t/t/articles2003/03 Ghosn (16/2/2012).

Githiora, B. (1979). "The Influence of Literature of Young Children's Concept Formation"Tasnifu ya M.A. University of Nairobi. (Haijachapishwa).

Gituku, N. (1990). "Maigizo ya kienyeji ya Watoto Nchini Kenya" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapichwa).

Good, C. (1972). *Essentials of Education: Research Methodology and Design*. New York: Meredith Corporation.

Hawkes, T. (1977). *The Structuralism and Semiotics*. London: Metheun.

Holindale, P. (1974). *Choosing Books for Children.* London: Paul Elek Ltd.

Huck, C. (1979). *Children's Literature in the Elementary School*. New York: Oxford University press.

Huck, C. S. (1979). *Children's Literature in the Elementary School* (3rd ed). New York: Holt and Winston.

Hudson, W. H. (1972). *An Introduction to the Study of Literature*. Oxford: Oxford University Press.

Hunt, P. (1996). *International Companion: Encyclopeadia of Children Literature.* London: Routledge. (pp. 1 – 29).

Hurst, C. & Rebecca O. (2004). *Carol Hurst's Children Literature Site*. Retrieved from: http//www//carolhurst.com 13.8.2012.

Ipara, J. P. (2004). “Matatizo ya Kufundisha Fasihi Simulizi katika Shule za Sekondari”. Makala yaliyowasilishwa katika kongamano la CHAKITA juu ya Historia, Maendeleo na Mustakabali wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili.

Islam, K.I., Kyoi, P.K., Mungai, J & Musembi, N. (2009). *Dhibiti PTE Kiswahii*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.

Jan, I. (1969). *Children's Literature*. London: Trinity Press.

John, J.& Davis, J. (1990). *Integrating Literature into Middle School Reading Classroom*. Retrieved from: http//www.ericdigest.org/pre9214/middle.html 22.10.2012.

Kahenya, P. W. (1992). “Children's Literature an Analytical Study of the Content Value of Tin Tin Comic*”*Tasnifu ya M.A., Thesis University of Nairobi (Haijachapishwa).

Kairu, W. M. (2005). “Uhalisi na Mtindo wa Ken Walibora katika ‘Fasihi ya Watoto”, Tasnifu ya M.A., Kenyatta University. (Haijachapishwa).

Kang'ahi, M. (2012). Teaching Styles and Learners' Achievement in Kiswahili Language in Secondary Schools. *International Journal of Academic Researchin Progressive Education and Development*. July 2012, Vol. 1..

Karuga, M. N. (2005). “Uhakiki wa Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika Shule za Msingi nchini Kenya”, Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kenya Institute of Curriculum Development (2002). *Primary Education Syllabus* (Vol. 1). Nairobi: K.I.C.D

King'ei, G. K. (2012). *Language Provisions in Kenyas' New Constitution and their Implication on Language Policy* in *Kiswahili (Vol. 75)*. Dar es Salaam: TUKI.

Knowles, M. (1996). *Language and Control in Childre's Literature*. New York: Harper Collins

Kombo, K. & Tromp, A. L. D. (2006). *Proposal and Thesis Writing; An Introduction.* Nairobi: Pauline Publications Africa.

Konrad, G. (2008). *Promoting a Culture of Reading in Kenya*. Available: lowlune/htt/www. 10.8.2012

Leech, G. H. & Short, M. H. (1981). *Style in Fiction a Linguistic Introduction to English Fiction Prose*. England: Longman Group.

Lesnik – Obsertein, K. (1996). Defining Children's Literature and Childhood. In Peter Hunt (ed.) *International Companion Encyclopaedia of Children's Literature*. London: Routledge. (pp.17 – 31).

Lukens, J. (1982). *A Critical Handbook of Children's Literature*. Boston: Pearson Education, Inc.

Lukens, R. (1995). *A Critical Handbook of Children's Literature*. New York: Harper Collins.

Magara, E.& Batambuza, C. (2005). Towards a Reading Culture for Uganda. *African Journal of Library Archive and Information Science*, Vol. 15 No. 1

Marrow, L. & Gambrell, L. (2001). Literature based instruction in the early years in S.B Neumaina D.K Dickison (eds). *Handbook of early literacy research* pp 348-360. New York: Gullford Press.

Massamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500 BK*. Nairobi.: Jomo Kenyatta Foundation.

Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Africa: A Dependency Theory Perspective.* Nairobi. Educational Research and Publications (ERAP).

Mbae, J. (2004). Kenya: A Reading Nation. In Wajibu. *Journal of Social and Religious Concern*. Retrived from: http://africa.peacelink.org/wajibu/articles/art 4487 html (3/4/2012).

Ministry of Education (2002). *Ministry of Education and Technology's Primary School Education Syllabus (Vol. 1).* Nairobi: Ministry of Education.

Momanyi, C. (2007). Nafasi ya Lugha ya Kiswahili katika Elimu ya Vyuo Vikuu nchini Kenya. In Njogu K.(Mh.) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya* Nairobi: Twaweza Communications (kur. 3-19)

Mpesha, N. (1995). "Children's Literature in Tanzania: A Literary Appreciation of its Growth and Development"Tasnifu ya PhD. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: TUKI.

Mugenda, O.M. & Mugenda, A. G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.

Mukwa, C. W. (1988). *Educational Communication and Technology Pan II.* Nairobi: Nairobi University Press.

Muthubi, F. (2005).“Mikakati na Mbinu za Usimilishwaji katika Fasihi ya Watoto” Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Muthwi, M. (2004). Language of Instruction: A Qualitative Analysis of the Perception of Parents, Pupils and Teachers among the Kalenjin in Kenya, *Language Culture and Curriculum* 17, 15-32.

Mwanza, P.M. (2007). “Mtindo wa Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea”, Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu chaKenyatta. (Haijachapishwa)

Mwanzi, H. O. A. (1982). “Children’s Literature in Kenya: An Analysis of Children Prose Fiction”, Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Nagler, M. N. (1974). *Spontaneity and Tradition: A Study in Oral Art of Homer.* Barkeley: University of California Press.

Ng’ong’a, B. (2002). “An Assessment of English Language Teacher Education in the Light of Classroom Needs: A Case Study of Maseno University” Tasnifu ya PhD. Maseno University. (Haijachapishwa).

Ngugi, P. M. (2009). “Language and Literary Education. The State of Children’s Literature in Kiswahili in Primary Schools in Kenya”, Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Wien (Haijachapishwa).

Ngunjiri, J. (2007). *Kenya’s Best-Selling Authors and Titles*, Sunday Nation, September, 9, 2007. Nairobi. Nation Media Group Ltd.

Nicholas, T. (1981). *The Child and the Book: A Psychological and Literary Explorations.*Cambridge: Cambridge University Press.

Njogu, K. & Chimera R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Odaga, A. B. (1974). “Literature for Children and Young People”, Tasnifu ya B.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Odaga, A. B. (1985).*Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi. Nairobi University Press

Ornstein A. C. & Hunkins, F. P. (2004). *Curriculum Foundations Principle and Issues* 4th ed. New York: Pearson Education Inc.

Osazee, F.P. (2004). *Not Only Books for Africa but A Reading Culture Too. Keynote Address Presented at the 29th IBBY Congress*. Cape Town. South Africa 5-9th September 2004. http.//www/saclof.org.za/2004/20% papers/osazee%20fayose rtf. Downloaded 8/12/2012.

Otim, R. (2000). *An Endangered Subject: The Role of Literature in English in National Integration and Development*. In Kate Parry (ed.) Language and Literacy in Uganda: Towards a Sustainable Reading Culture. Kampla: Fountain Publishers.

Oyoo, M. (2003). *Theory of Children's Literature (Module).* Nairobi: Catholic University of Eastern Africa, Literature Department.

Pawlitzky, C. (2005). "High Reputationlow Priority Reading Habits in Multilingual Kenya" PhD Dissertation. Universitat. Humburg.http//deposit.d.nb.ddcg.in/dokserv?idn=9777.

Ray, G. (1970). *Children's Fiction: A Handbook for Librarians*. Leicester: Brockhampton Press.

Reese, D. A & Harris, V. J. (1997). *Look at this nest: The beauty and Power Children Early Child Development and Care*, 127 – 128, 217 – 131. Routledge.

Ruddell, R.B. (2002). *Teaching Children to Read and Write Becoming and Effective Literacy Teacher* (3rd ed). New York: Allyn and Bacon.

Saunders, D. J. (1974). *Visual Communication Handbook: Teachig and Learning Using Simple Visual Materials*. London: Lutterworth Press.

Scholes, R. (1974). *Structuralism in Literature: An Introduction*. New Haven: Yale University Press.

Senkoro, F. (1982). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Sifuna, N.D. (1991). Difersifying the Secondary School Curriculum. The African Experience. Nairobi: Bureau Educational Research.

Southerland, Z. (1997). *Children and Books.* New York: Longman.

Stewig, J.W. (1980). *Children and Literature*. Chicago: Rand Mc Nally College Publishing Company.

Stict – Gohdes, W.L. (2001). Business Education. Students' Preferred Learning. Styles and their Teachers' Preferred Instructional Styles: Do they Match? *Delta P. Episilon Journal*. 43 (3) 137 – 151.

Sverby, K. E. (1997). *The New Organizational Wealth: Managing and Measuring Organizational Wealth*. San Francisco: Berret Koehle

Tucker, N. (1982). *The Child and the Book*. New York: Cambridge University Press.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Weche, M.O. (2002). "Children's Literature as an Image Force. A Case Study of Ezekiel Alembi's Books" Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Weinreich, T, & Bartlett, D. (2000). *Children's Literature: Art or Pedagogy.* Rosttilde: Rosttilde University Press.

Wills, B. J. (1988). Aspects of the Acquisition of Orality and Literary in Kenyan Primary School Children. *Kiswahili Disseration Abstracts International* 50,433, Umino 8908590.

Wright, A. (1976). *Visual Materials for Language Teachers*. London: Longman Publishers.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Hojaji ya walimu

Hojaji hii inatarajiwa kupata habari kuhusu mikakati inayotumiwa na walimu katika ufundishaji wa kusoma fasihi ya watoto ya Kiswahili. Ujumbe utakaopatikana utatumiwa kuwaelekeza wanafunzi katika kupenda kusoma na kufanya mitihani yao vizuri. Taarifa zote zitazingatiwa kwa usiri mkubwa. Tafadhali jaza katika visanduku kwa kuweka alama ya mkwaju [ √ ] kwa jibu mwafaka au utoe jibu kamili kulingana na maagizo.

1. Jinsia ya Mwalimu:
   - Mke [ ]
   - Mume [ ]
2. Miaka ya mwalimu ni:
   - Chini ya miaka 20 [ ]
   - Miaka 21-30 [ ]
   - Miaka 31-40 [ ]
   - Miaka 41-50 [ ]
   - Miaka 51-60 [ ]
3. Kiwango cha masomo uliyonayo ya juu ni:
   - Shahada [ ]
   - Diploma [ ]
   - Cheti cha ualimu [ ]
   - Hauna kozi [ ]
4. Umesoma kozi yoyote ile ya kukusaidia katika ufundishaji wako wa fasihi ya watoto ulipokuwa katika chuo cha ualimu
   - Ndio [ ]
   - Hapana [ ]

Kama ndio eleza ni ipi ______________________________________________

______________________________________________________________

5. Umefundisha kwa miaka mingapi?
   - Miaka 0-5 ☐
   - Miaka 6-10 ☐
   - Miaka 11-15 ☐
   - Miaka 15-20 ☐
   - Zaidi ya miaka 20 ☐
6. Unafundisha vipindi vingapi kwa wiki
   - Vipindi 20-25 ☐
   - Vipindi 26-30 ☐
   - Vipindi 31-35 ☐
   - Vipindi36-40 ☐
7. Ni vipindi vingapi vimetengewa somo la Kiswahili katika darasa la saba kwa wiki?
   - Kimoja ☐
   - Viwili ☐
   - Vitatu ☐
   - Vinne ☐
   - Vitano ☐
8. Ni vipindi vingapi vimetengewa somo la kusoma fasihi ya Kiswahili katika darasa la saba
   - Kipindi kimoja ☐
   - Vipindi viwili ☐
   - Vipindi vitatu ☐
   - Vipindi zaidi ☐

   Iwapo ni vipindi zaidi taja idadi ☐

9. Katika sehemu hii weka alama ya mkwaju [ √ ] kwa mikakati unayotumia katika ufundishaji wa kusoma fasihi ya Kiswahili

| **Mikakati ya ufundishaji** | **Kila wakati** | **Mara mojamoja** | **Situmii kabisa** |
|---|---|---|---|
| Usomaji wa kipekee | | | |
| Usomaji wa pamoja | | | |
| Usomaji wa unachopenda | | | |
| Usomaji wa kimya | | | |
| Usomaji kwa sauti | | | |
| Fasihi ya mzunguko | | | |

10. Wanafunzi hupendelea mikakati gani inayotumiwa katika ufundishaji wako

Kusoma kwa sauti ☐

Kusoma kwa pamoja ☐

Kusoma kimya ☐

Kusoma unachopenda ☐

Kwa maoni yako ni mikakati gani ambayo husaidia wanafunzi katika umilisi wa kusoma ____________________________________________

____________________________________________

11. Ni mambo gani ambayo hutatiza ufundishaji wa fasihi ya watoto darasani?

(i) Mwelekeo wa mwalimu ☐

(ii) Idadi ya wanafunzi darasani ☐

(iii) Kitabu kinachosomwa darasani ☐

(iv) Muda wa kusoma ☐

(v) Mikakati isiyofaa ☐

12. Hapa chini kuna baadhi ya vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wa fasihi katika shule za msingi. Onyesha vifaa unavyotumia kwa kuweka alama mkwaju ya [√] kuonyesha unavyovitumia

| Vifaa | Kila Wakati | Mara Mojamoja | Havitumiki |
|---|---|---|---|
| Radio | | | |
| Ubao | | | |
| Runinga | | | |
| Filamu | | | |
| Magazeti | | | |
| Vitabu vya hadithi | | | |
| Picha | | | |
| Vinasa sauti | | | |
| Mabango | | | |

13. Ni mambo gani yanayoathiri uteuzi wa vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wa fasihi ya watoto (weka alama ya mkwaju [√]katika visanduku vya majibu yako)

(i) Urahisi wa kupatikana kwa vifaa ☐

(ii) Namba ya wanafunzi darasani ☐

(iii)Bei ya vifaa hivyo ☐

(iv)Ugumu wa kuvitumia vifaa hivyo ☐

14. Je, unatumia zaidi ya kifaa kimoja katika ufundishaji wako? (weka alama ya mkwaju [√]katika kisanduku)

Ndio ☐

La ☐

Kama jibu ni ndio, eleza ______________________________________________

______________________________________________________________

Kwa kifupi eleza manufaa yanayotokana na kutumia vifaa katika ufundishaji wa kusoma__________________________________________________________

______________________________________________________________

15. Ni shughuli gani ambazo wanafunzi hujihusisha nazo unapofundisha?
(weka alama ya mkwaju [√]katika kisanduku)

(i) Kujibu maswali ☐

(ii) Kujadiliana ☐

(iii) Kuigiza ☐

(iv) Kuandika muhtasari ☐

(v) Kueleza kwa muhtasari ☐

16. Kwa maoni yako kama mwalimu, shughuli hizo za mwanafunzi humsaidia katika usomaji

Ndio ☐

La ☐

Ikiwa jibu lako ni ‘la’, tafadhali toa maelezo mafupi

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

17. Ni mara ngapi unawapatia wanafunzi zoezi la kusoma kwa sauti

(i) Kila siku ☐

(ii) Mara moja kwa wiki ☐

(iii) Baada ya wiki mbili ☐

(iv) Baada ya mwezi ☐

(v) Siwapatii ☐

18. Je, ulifundishwa mbinu za ufundishaji wa fasihi ya watoto katika chuo cha ualimu?

Ndio ☐

La ☐

Iwapo jibu ni ‘ndio’, taja mbinu tatu ulizojifunza

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

19. Ni lugha gani hutumiwa miongoni mwa wanafunzi katika shule unayofundisha

Darasa la 1 – 3 ____________________________________________________

Darasa la 4 – 8 ____________________________________________

Kwa kifupi eleza manufaa ya lugha hiyo (hizo) zinavyotumika katika kuimarisha kiwango cha usomaji wa vitabu vya hadithi shuleni.

______________________________________________________________

______________________________________________________________

20. Je, wewe hushiriki katika kuchagulia wanafunzi vitabu vinavyotumiwa shuleni?

Ndio ☐

La ☐

Ikiwa jibu lakoni 'ndio' eleza kwa kifupi sababu zinazozingatiwa

______________________________________________________________

______________________________________________________________

21. Je, vitabu vinavyotumiwa shuleni kwenu huchaguliwa na nani?

Taasisi ya elimu (KICD) ☐

Mwalimu mkuu ☐

Wazazi ☐

Mwalimu wa darasa ☐

22. Katika shule unayofundisha kuna maktaba?

Ndio ☐

La ☐

Iwapo jibu lako ni 'la', eleza kwa kifupi sababu yenyewe

______________________________________________________________

______________________________________________________________

23. Kwa maoni yako ni vitabu vingapi vya fasihi ya watoto hupatikana katika maktaba hiyo? (unaweza kukadiria tu)

0 – 10 ☐

10 – 20 ☐

30 – 40 ☐

Zaidi ya 50 ☐

24. Ni vitabu vingapi wewe kama mwalimu wa Kiswahili huvitumia darasa ni katika muhula mmoja

1 – 5 ☐

5 – 10 ☐

10 – 20 ☐

20 – 30 ☐

Zaidi ya 30 ☐

25. Je ni wanafunzi wangapi huomba uwapatie vitabu vya hadithi ili wavisome?

Wote huuliza ☐

Wachache ☐

Wengi ☐

Hakuna anayeuliza ☐

Iwapo hawaombi, eleza kwa kifupi sababu yenyewe

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## Kiambatisho II: Kutazama somo darasani

Shule ______________________________ Mada __________________________

Darasa ______________________________ Tarehe _________________________

1. Ratiba ya kazi

   Ipo ☐

   Haipo ☐

2. Mpangilio wa kazi

   Upo ☐

   Haupo ☐

3. Ujuzi wa mwalimu

   Mzuri zaidi ☐

   Mzuri ☐

   Wastani ☐

   Usioridhisha ☐

4. Mikakati inayotumiwa na mwalimu katika ufundishaji

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

5. Mikakati hiyo inatumiwa vilivyo?

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

6. Taja vifaa mwalimu anavyotumia katika ufundishaji wake

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

7. Mwalimu hutumia vifaa hivyo vipi?

- Vizuri zaidi ☐
- Vizuri ☐
- Wastani ☐
- Hairidhishi ☐

8. Vifaa vya ufundishaji vinatumiwa wakati gani katika somo?

- Mwanzoni mwa somo ☐
- Katikati mwa somo ☐
- Anapomalizia somo ☐

9. Ni shughuli gani katika somo ambazo mwalimu huwashughulisha wanafunzi zaidi?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

10. Je, mwalimu huwapa wanafunzi zoezi lolote?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**Kiambatisho III: Mwongozo wa maswali ya mahojiano na walimu wa kiswahili darasa la saba**

1. Kwa nini unapenda kufundisha fasihi ya Kiswahili?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

2. Wewe, hufanya matayirisho yapi katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

3. Je, wanafunzi wako hupenda kusoma vitabu vya fasihi ya Kiswahili. Ni kwa nini wanapenda au hawapendi?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

4. Ni jambo gani hasa hukupatia msukumo wa kufundisha kusoma fasihi ya watoto?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

5. Ni matatizo gani wewe hukabiliana nayo unapofundisha fasihi darasani (Tafadhali jaza kwa kutumia alama ya mkwaju katika visanduku vilivyopo)

| | |
|---|---|
| Darasa kubwa | ☐ |
| Kukosa vifaa | ☐ |
| Kukosa muda wa kutosha | ☐ |
| Ukosefu wa vitabu | ☐ |

6. Ni vifaa gani vya ufundishaji ambavyo vinapatikana kwa urahisi shuleni kwenu?

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

7. Ni mara ngapi wewe kama mwalimu hutumia vifaa hivi katika ufundishaji wa kusoma

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

8. Je, fasihi ya Kiswahili ya watoto ina manufaa gani au yapi katika kuimarisha kiwango cha lugha ya Kiswahili? Tafadhali eleza kwa kifupi

_______________________________________________________________

## Kiambatisho IV: Matokeo ya uchambuzi wa insha za wanafunzi

| Mwanafunzi | Alama alizotuzwa 40/40 | Uakifishaji 3/40 | Tahajia 3/40 | Msamiati 12/40 | Uwasilishaji wa ujumbe 14/40 | Mpangilio na mtindo 8/40 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 18 | 1 | 1 | 4 | 7 | 5 |
| 2 | 16 | 0 | 0 | 5 | 7 | 4 |
| 3 | 20 | 1 | 1 | 4 | 8 | 6 |
| 4 | 21 | 0 | 1 | 6 | 7 | 7 |
| 5 | 15 | 0 | 1 | 5 | 5 | 4 |
| 6 | 14 | 0 | 1 | 4 | 6 | 3 |
| 7 | 05 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0 |
| 8 | 22 | 2 | 2 | 6 | 7 | 4 |
| 9 | 15 | 0 | 0 | 6 | 7 | 2 |
| 10 | 17 | 1 | 1 | 5 | 6 | 4 |
| 11 | 16 | 1 | 1 | 4 | 7 | 3 |
| 12 | 23 | 1 | 1 | 8 | 8 | 5 |
| 13 | 28 | 2 | 2 | 9 | 8 | 6 |
| 14 | 12 | 1 | 1 | 3 | 5 | 2 |
| 15 | 19 | 1 | 1 | 5 | 7 | 5 |
| 16 | 22 | 2 | 2 | 6 | 8 | 5 |
| 17 | 10 | 0 | 0 | 2 | 5 | 4 |
| 18 | 05 | 0 | 0 | 1 | 3 | 1 |
| 19 | 25 | 2 | 2 | 8 | 8 | 5 |
| 20 | 20 | 1 | 1 | 6 | 8 | 5 |
| 21 | 22 | 2 | 2 | 6 | 7 | 4 |
| 22 | 14 | 0 | 0 | 3 | 7 | 4 |
| 23 | 11 | 0 | 0 | 3 | 6 | 3 |
| 24 | 21 | 2 | 2 | 5 | 8 | 5 |
| 25 | 17 | 1 | 1 | 4 | 7 | 4 |
| 26 | 07 | 0 | 0 | 1 | 4 | 2 |
| 27 | 26 | 2 | 2 | 8 | 9 | 5 |
| 28 | 30 | 2 | 2 | 9 | 10 | 6 |
| 29 | 13 | 0 | 0 | 3 | 6 | 4 |
| 30 | 14 | 0 | 0 | 4 | 5 | 5 |
| 31 | 24 | 2 | 2 | 7 | 8 | 5 |
| 32 | 24 | 1 | 1 | 8 | 9 | 5 |
| 33 | 26 | 2 | 2 | 8 | 8 | 6 |
| 34 | 22 | 1 | 1 | 6 | 8 | 6 |
| 35 | 24 | 1 | 1 | 8 | 9 | 3 |
| 36 | 24 | 2 | 2 | 9 | 8 | 4 |
| 37 | 25 | 2 | 2 | 8 | 8 | 5 |
| 38 | 19 | 1 | 1 | 6 | 8 | 3 |
| 39 | 24 | 2 | 2 | 7 | 8 | 5 |
| 40 | 26 | 2 | 2 | 8 | 9 | 6 |
| 41 | 20 | 1 | 1 | 6 | 8 | 4 |
| 42 | 19 | 1 | 2 | 5 | 7 | 4 |
| 43 | 19 | 0 | 1 | 5 | 8 | 5 |
| 44 | 15 | 0 | 0 | 4 | 6 | 5 |
| 45 | 24 | 2 | 2 | 7 | 7 | 6 |
| 46 | 25 | 2 | 2 | 6 | 8 | 7 |
| 47 | 21 | 2 | 1 | 5 | 9 | 4 |
| 48 | 16 | 0 | 0 | 4 | 7 | 5 |
| 49 | 15 | 1 | 1 | 4 | 6 | 3 |
| 50 | 12 | 1 | 0 | 3 | 4 | 4 |
| 51 | 14 | 0 | 1 | 3 | 5 | 5 |
| 52 | 24 | 2 | 1 | 8 | 7 | 6 |
| 53 | 10 | 0 | 0 | 1 | 6 | 3 |
| 54 | 21 | 1 | 1 | 6 | 8 | 5 |
| 55 | 05 | 0 | 0 | 6 | 3 | 2 |
| 56 | 20 | 1 | 1 | 5 | 8 | 5 |
| 57 | 13 | 1 | 1 | 4 | 5 | 2 |
| 58 | 17 | 0 | 0 | 5 | 8 | 4 |
| 59 | 09 | 0 | 0 | 2 | 4 | 3 |
| 60 | 19 | 1 | 1 | 6 | 7 | 5 |

**Kiambatisho V: Barua ya idhini (NACOSTI)**

NACOSTI

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone: +254-20-2213471, 2241349, 310571, 2219420
Fax: +254-20-318245, 318249
Email: secretary@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke
When replying please quote

9th Floor, Utalii House
Uhuru Highway
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No.

Date:

**8th January, 2015**

**NACOSTI/P/14/2042/4322**

Selina Rhobi Chacha
Kenyatta University
P.O. Box 43844-00100
**NAIROBI.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Uchanganuzi wa mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili na umilisi wa kusoma katika shule za msingi, Kaunti ya Nairobi, Kenya,"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Nairobi County** for a period ending **5th June, 2015.**

You are advised to report **the County Commissioner and the County Director of Education, Nairobi County** before embarking on the research project.

On completion of the research, you are required to submit **two hard copies and one soft copy in pdf** of the research report/thesis to our office.

**SAID HUSSEIN**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Nairobi County.

The County Director of Education
Nairobi County.

*National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO 9001: 2008 Certified*


## Kiambatisho VI: Cheti cha idhini (NACOSTI)

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MS. SELINA RHOBI CHACHA***
**of KENYATTA UNIVERSITY, 7545-300 nAIROBI,has been permitted to conduct research in *Nairobi County***

**on the topic: *UCHANGANUZI WA MIKAKATI YA UFUNDISHAJI WA FASIHI YA KISWAHILI NA UMILISI WA KUSOMA KATIKA SHULE ZA MSINGI,KAUTI YA NAIROBI, KENYA***

**for the period ending:**
***5th June,2015***

**Permit No : NACOSTI/P/14/2042/4322**
**Date Of Issue : 8th January,2015**
**Fee Recieved :Ksh 1,000**



.................................
***Applicant's Signature***

.................................
***Secretary***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

**CONDITIONS**

1. **You must report to the County Commissioner and the County Education Officer of the area before embarking on your research. Failure to do that may lead to the cancellation of your permit**
2. **Government Officers will not be interviewed without prior appointment.**
3. **No questionnaire will be used unless it has been approved.**
4. **Excavation, filming and collection of biological specimens are subject to further permission from the relevant Government Ministries.**
5. **You are required to submit at least two(2) hard copies and one(1) soft copy of your final report.**
6. **The Government of Kenya reserves the right to modify the conditions of this permit including its cancellation without notice**

**REPUBLIC OF KENYA**

NACOSTI

**National Commission for Science, Technology and Innovation**

**RESEARCH CLEARANCE PERMIT**

**Serial No. A** 3974

**CONDITIONS: see back page**